SUPA JACKPOT
TZS. 1,074,741,067
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Kauli** tata ya Mwigulu yaibua jambo bungeni

UKURASA 3


PAJUE MAKARAI MWANZA – FUNDI HALALI NJAA!
Kiwanda kidogo kilichosheheni mafundi mchundo, siri ajira binafsi, darasa la mamia mafundi wapya
Ukurasa 12
Usuluhishi wa migogoro uwe wa lazima
Ukurasa 13
BUFE
IJUMAA FEBRUARI 10, 2023 Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Ijue PPRA inavyosimamia zabuni ya ununuzi umma, hadi utekezaji
Ukurasa 14
UCHUMI
Rais alipoelekeza urafiki na walipa kodi, ikamjibu na pato rafiki kitaifa
Na Mwandishi Wetu
• Hakuna biashara kufungiwa, azuia riba kodi ardhi...

UKURASA 11

# Nipashe

Ijumaa Februari 10, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581217

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



Wananchi wakiangalia mabaki ya basi la abiria la kampuni ya Frester lililokuwa likitokea Bukoba kwenda Dar es Salaam na lori lililobeba shehena ya saruji, baada ya kugongana katika barabara kuu ya Morogoro-Dodoma, eneo la Silwa mkoani Dodoma na kusababisha vifo vya watu 12 na wengine zaidi ya 50 kujeruhiwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ajali mpya ilivyowaua abiria 12 na kujeruhi 63

• **Wamo** askari waliosafirisha mtuhumiwa... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**LISSU AFUATA GARI POLISI ALIWEKE MAKUMBUSHO**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA)...

## Bunge lataka hatua kasi kuzagaa PhD za mchongo

UKURASA 3



Baadhi ya magari yakipita kwa tabu katika Barabara ya Morogoro, eneo la Jangwani, kutokana na mafuriko yaliyosababishwa na mvua kubwa iliyonyesha mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Umeme wakwamisha huduma Muhimbili kwa saa tano

UKURASA 2

**MICHEZO** NABI APATA MBINU KUIUA US MONASTIR UK.24

**KATUNI** UK.6



Mwenyekiti wa kijiji cha Mwarimba, kata ya Misozwe, wilayani Muheza, mkoani Tanga, Rogers Kanju (wa pili kulia), akitoa maelezo kwa askari polisi, kabla ya kuanza kufyeka dawa za kulevya aina ya bangi, zilizopandwa kwenye shamba la mihogo la Elia Jilali Kunguru, kijijini hapo jana. Kushoto ni Mkuu wa upelelezi wa makosa ya jinai wa wilaya hiyo, Charles Ntenga. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Umeme wakwamisha huduma MNH kwa saa tano

**Na Waandishi Wetu**

MVUA kubwa iliyonyesha usiku wa kuamkia jana imesababisha usumbufu na maafa katika maeneo mbalimbali hususan mkoani Dar es Salaam, huku watu wanaotibiwa katika jengo jipya la wagonjwa wa nje (New OPD) katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) wakikosa huduma kwa zaidi ya saa tano.

Kukosekana kwa huduma hiyo kulisababishwa na kukosekana kwa umeme katika jengo hilo. Hatua hiyo pia ilisababisha baadhi ya wagonjwa kulazimika kurudi nyumbani huku waliokwenda kufuata majibu wakiambiwa na madaktari warudi wiki ijayo.

Mmoja wa wagonjwa waliokwenda kupata huduma, Mariam Chande, mkazi wa Mtoni kwa Azizi Ally, aliiambia Nipashe kuwa ameshindwa kupewa majibu aliyopima mwezi uliopita kwa sababu kompyuta hazifanyi kazi kutokana na kukosekana kwa umeme.

"Niko hapa tangu saa 2:15 asubuhi na sasa hivi ni 6:30, sijapewa majibu na tuko wengi. Daktari ameniambia niendelee kusubiri mpaka umeme utakaporudi lakini hata yeye hajui utarudi saa ngapi," alisema.

Nuru Kondo, Mkazi wa Kiwalani, Manispaa ya Ilala, aliyempeleka mtoto wake kupima damu, alisema anasikitishwa na kitendo cha uongozi kutowapa taarifa yoyote kuhusu upatikanaji wa huduma hiyo kutokana na hitilafu hiyo, hali iliyowafanya wakae bila kujua kinachoendelea.

"Kinachosikitisha ni kuwa tumekaa tu bila kuambiwa kuwa hii hitilafu inafanyiwa kazi au tuondoke turudi kesho (leo). Leo (jana) mtoto amekosa masomo siku nzima. asipopata huduma itabidi na kesho tuje tena, ina maana atakosa tena masomo," alisema Kondo.

William Poyongo, Mkazi wa Kigoma aliyepeleka mtoto wake, alisema kutokana na hitilafu hiyo, daktari aliwaambia warudi Alhamisi ijayo kuchukua majibu waliyopima siku kadhaa nyuma jambo alilosema analiona si sahihi.

"Tumeingia kwa daktari akatuambia kuwa hataweza kutusomea majibu leo kwa sababu umeme hakuna kwa hiyo turudi tena Alhamisi ijayo. Kwangu mimi naona kama si sawa. Ina maana huo umeme hautarudi hadi Alhamisi ijayo? Kwa nini asituambie tuje kesho? alihoji.

Poyongo alisema kitendo cha kutakiwa kurudi wiki ijayo kinamrudisha nyuma kimaendeleo kwa kuwa alifunga biashara zake Kigoma kwenda Dar es Salaam kumuuguza kijana wake, akitegemea kurudi mapema wiki ijayo ili akaendelee na shughuli zake.

Kutokana na danadana hiyo, alisema fedha zote alizopanga kutumia ndani ya mwezi mmoja akiwa Dar es Salaam zimekwisha, hivyo atalazimika kuomba ndugu na jamaa wamsaidie ili akae hadi wiki ijayo.

**MAJIBU YA UONGOZI**

Saa 7:30 mchana, Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Mohammed Janabi, alitoa majibu kwamba chanzo cha tatizo hilo ni hitilafu ya umeme iliyotokana na mvua zilizonyesha usiku wa kuamkia jana. Hata hivyo, alisema kwa wakati huo mafundi walikuwa wameshatatua tatizo hilo na huduma zinaendelea kama kawaida.

"Umeme ulikatika tukawasha jenereta, likafanya kazi kidogo nalo mkanda ukakatika. Wakati wanalirekebisha na TANESCO (Shirika la Umeme Tanzania) nao wakawa wameshafika kurekebisha hitilafu, kwa hiyo huduma zinaendelea kama kawaida," alisema Prof. Janabi.

**ATHARI ZAIDI MVUA**

Wakati hali ikiwa hivyo Muhimbili, mvua hiyo kubwa iliyonyesha usiku kucha, ilisababisha athari zaidi ikiwamo baadhi ya shughuli za maendeleo kukwama huku katika baadhi ya maeneo maji yakiingia kwenye nyumba na kuharibu mali.

Nipashe ilitembelea baadhi ya maeneo na kushuhudia madaraja yakiwa yamefurika na kusababisha magari kushindwa kupita. Hali hiyo ililisababisha baadhi ya wakazi wa Dar es Salaam kutoa maji ndani ya nyumba na katika baadhi ya barabara kuwapo kwa foleni kubwa.

Moja ya maeneo yaliyokumbwa na tatizo hilo ni Tabata jijini Dar es Salaam, ambako baadhi ya wakazi walilazimika kuchelewa kufanya shughuli zinazowaingizia kipato baada ya kuwapo kwa foleni kubwa iliyosababishwa kufurika kwa daraja, eneo la Tabata Relini.

Nipashe ilishuhudia watu wakiacha magari na kuvuka kwa miguu kisha kupanda magari yaliyoko upande wa pili na kuendelea na safari huku makondakta wa daladala wakiwabeba wanafunzi kuwavusha upande wa pili ili kuwaepusha na madhara ikiwamo kusombwa na maji.

Doroth Paul, mkazi wa Kinondoni, Dar es Salaam, alisema alichelewa kufungua biashara yake ya kuuza viatu Kariakoo baada nyumba yake kujaa maji yaliyopitia chini ya ardhi.

Alisema ni kawaida kwa nyumba anayoishi kuingia maji mvua zinapokuwa kubwa yakitokea nje kwa kuwa hakuna mitaro ya kupitisha maji.

"Tumeshazoea hali hii. Haya maji yanaingilia kwa chini na yanajaa ndani. Wakati mwingine yanafika hadi usawa wa kitanda, kwa hiyo hapa tunayatoa nje kisha tusafishe nyumba ndiyo niende kwenye shughuli zangu," alisema.

**VINYAGO MWENGE**

Katika eneo la Mwenge Vinyago, kulijaa maji kwenye baadhi ya maduka, mengine yakiwa yamefikia kwenye kingo ambako hakuwezi kupitika kwa wateja kuingia ndani.

Baadhi ya wafanyabiashra katika eneo hilo, walisema eneo hilo lina miaka mingi tangu lianze kujaa maji na hakuna jitihada zozote zilizofanyika kuwasaidia.

"Eneo hili linajaa maji kwa miaka mingi sasa na hili lilianza tangu barabara ilivyonyanyuliwa. Kwa hiyo kila mvua inaponyesha maji hujaa na inapotokea hivyo, hakuna biashara kabisa,"alisema Neema Mbutaki mmoja wa wafanyabiashara katika eneo hilo.

Maeneo mengine ambayo Nipashe ilishuhudia maji yakiwa yamejaa ni barabara ya Pamba iliyopo Posta, Tandale, na Jangwani.

**-Imeandikwa na Jenifer Gilla na Elizabeth Zaya, DAR.**

# Ajali nyingine ilivyoa watu 12

**Augusta Njoji na Idda Mushi**

UZEMBE na mwendokasi wa dereva wa basi la Kampuni ya Frester umetajwa kuwa chanzo cha ajali iliyosababisha vifo vya watu 12 na majeruhi 63 kwenye kijiji cha Silwa barabara kuu ya Dodoma-Morogoro jana.

Katika ajali hiyo, askari polisi wawili waliokuwa wakisafirisha mtuhumiwa ni miongoni mwa walipoteza maisha.

Ajali hiyo ilitokea usiku wa kuamkia jana baada ya basi hilo lenye namba T415 DPP kugongana uso kwa uso na lori lililokuwa na shehena ya saruji lenye namba za usajili T 677 DVX kijijini huko wilayani Kongwa.

Tukio hilo la vifo vya watu wengi kutokana na ajali limetokea ikiwa ni siku sita tangu kutokea kwa ajali nyingine ya basi dogo la abiria lililokuwa linasafirisha mwili kwenda Rombo mkoani Kilimanjaro, kugongana na lori la mzigo wilayani Korogwe mkoani Tanga Februari 3 mwaka huu na kusababisha vifo vya watu 20, wakiwamo ndugu 16.

Mkuu wa Operesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi, Kamishna Awadh Haji ni miongoni mwa viongozi waliofika eneo la ajali na kusema chanzo cha ajali hiyo ni mwendokasi na uzembe wa dereva wa basi hilo kutaka kulipita gari la mbele bila kuchukua tahadhari na kugongana na lori.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alitoa rai kwa jamii kutii sheria bila shuruti ili kuepuka ajali.

"Serikali ilikuwa na nia njema ya kuruhusu vyombo vya usafiri kutembea usiku, lakini sasa baadhi ya madereva wanaanza kutozingatia sheria za usalama barabarani, tutaendelea kuwachukulia hatua kali," alisema.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, Dk. Ernest Ibenzi alithibitisha kupokea majeruhi 15 wa ajali hiyo na kudai kuwa wengi wameumia kichwani na mikononi.

Alisema wanaendelea kuwapatia matibabu na wale watakaopata nafuu watawaruhusu kurudi nyumbani.

Mkuu wa Wilaya ya Kongwa mkoani hapa, Remidius Mwema alisema basi la Frester lililokuwa linatokea Bukoba mkoani Kagera kwenda Dar es Salaam na kwamba majeruhi 36 wako Hospitali ya Wilaya ya Gairo, huku majeruhi 27 wakipelekwa Kituo cha Afya Kibaigwa na wengine Dodoma kutokana na hali zao kuwa mbaya.

Miili ya watu 11 kati ya 12 waliofariki dunia kutokana na ajali hiyo, ilipokewa na kuhifadhiwa kwenye chumba cha kuhifadhi maiti cha Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro kwa ajili ya utambuzi.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Kessy Ngalawa alisema jana kuwa miongoni mwa miili hiyo, wamo wanawake watatu, wanaume saba na mwili mmoja wa mtoto wa jinsia ya kike anayekadiriwa kuwa na umri wa kati ya miaka minne hadi mitano.

Dk. Ngalawa alisema mpaka jana, miili ya watu wawili tu ndio iliyokuwa imetambuliwa kwa majina na utaratibu zaidi ulikuwa unaendelea ili kuwatambua marehemu wote waliopokewa kwenye hospitali hiyo.

Mmoja wa ndugu wa marehemu ambaye tayari mwili wake umeshatambuliwa Hamis Issa, alisema ndugu yake alikuwa askari polisi na aliongozana na askari mwenzake kumfuata mtuhumiwa ili kumpeleka jijini Dar es Salaam na kufikwa na umauti kwenye ajali hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Fatma Mwasa na kamati yake ya ulinzi na usalama ya Wilaya ya Gairo walifika eneo la ajali na Hospitali ya Wilaya ya Gairo na kutoa pole kwa wote waliofikwa na ajali na kuwashukuru watoa huduma za afya kwa kusaidia kutoa huduma licha ya tukio hilo kutokea mkoa mwingine.



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax akijibu maswali yaliyoulizwa na baadhi ya wabunge, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Bunge lataka hatua kasi PhD za mchongo

**Na Romana Mallya,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson ametahadharisha taifa kuhusu utolewaji wa shahada ya heshima, akionya kuwa itafika mahali wale wanaopewa kwa heshima inayostahili watakuwa hawana tofauti na wanaolipa fedha ili wapewe.

Pia amesema ni muhimu kama taifa kuweka mwongozo mzuri na viongozi kuwa mfano kwa watoto waliopo shuleni wasione kama shahada za heshima ni za kununuliwa.

Aliyasema hayo jana bungeni jijini Dodoma baada ya Mbunge wa Mlalo (CCM), Rashid Shangazi kuomba mwongozo wa Spika kuhusu shahada za heshima zilizotolewa kwa wabunge.

Katika mwongozo huo, mbunge huyo alitaka kufahamu ni kwa kiasi gani vyuo hivyo vinatambulika katika mamlaka za Tanzania zinazosimamia elimu, vigezo vya kuzitoa na kwa kiasi gani serikali inazitambua.

Suala hilo limeibuka zikiwa ni siku chache tangu Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, Hamis Taletale, maarufu kama Babu Tale, kutunukiwa shahada ya heshima na Academy of Universal Global Peace (AUGP-USA) ya Marekani.

Spika alisema kama taifa lazima wafike mahali wajue nini wanataka.

"Mheshimiwa waziri, umesema ninyi hamfuatilii yeyote anakopata lakini kama taifa athari zake tunaweza tusizione sasa, tutaziona baadaye kwa sababu hizi shahada za heshima zinazotolewa, tulishaelezwa kwa kirefu sana na Mheshimiwa (Palamagamba) Kabudi, ndiyo hasa lengo la kutolewa shahada za heshima," alisema.

Spika wa Bunge alisema Rais anapopewa udaktari wa heshima, lazima hufanyika utafiti wa kina kuhusu kazi alizozifanya, si tu alipokuwa Rais, tangu aanze kufanya kazi ambapo huzikusanya na hupitiwa kwa vigezo vya vyuo husika.

"Sasa tutafika mahali, wale wanaopewa kwa heshima wanayostahili hawana tofauti na hawa wanaolipa fedha ili wapewe hizo degree (shahada), sisi kama taifa lazima tufahamu utaratibu upi tunataka kwenda nao kwa sababu tusipofanya hivyo, tunajipoteza wenyewe hakuna mtu anayetupoteza.

"Sisi kama viongozi, lazima tuonyeshe mfano, mtoto wako umempeleka shule ili asome atie bidii, leo wewe kama mzazi unalipa fedha ili upewe 'degree' ya heshima, unampa mfano gani yule kijana aliyeko shule unayemkazania kusoma? "Kwamba, na wewe tafuta fedha ukishatafuta kalipe na wewe utapewa 'degree' ya heshima, umemtuma mtoto shuleni kufanya nini?" Spika alihoji. Spika alisema hilo analisema kwa jumla na kwamba halina uhusiano na wale waliopewa au kwamba wanalipa.

"Lakini, Mheshimiwa Waziri wakati anaeleza hapa sikutaka kuuliza maswali, ameweka tofauti ya chuo kinachotambuliwa na kisichotambuliwa, vyuo vinavyoteuliwa duniani huwa havitoi 'degree' kila wiki, kila mwezi, kila siku, kila mwaka na ninyi waheshimiwa wabunge si kazi yangu kuwaeleza lakini kafuatilieni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

"Kimeshawapa wangapi degrees za heshima, Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) kimewapa wangapi degrees za heshima.

"Si kwamba vyuo vya nje ndio vitumwagie degree za malipo halafu vya kwetu hapa havioni mchango wetu, waheshimiwa wabunge ni muhimu sana kwanza kama viongozi, pili kama taifa kuweka mwongozo mzuri kwa ajili ya wanaotufuata nyuma.

"Na mwongozo huo tutaweka vizuri tukifahamu Tanzania si kijiji, ni sehemu ya dunia nzima, huko zinakotoka hivyo vyuo wangeanza na nchi zao kugawia kila mtu degree, nilishawahi kupata ujumbe, ngoja nimhifadhi, yupo daktari wa kisomo humu ndani alisema 'tunakoelekea nadhani mimi nitaandika barua niache kutambuliwa kama daktari' kwa sababu hana tofauti yeye na huyu mwingine aliyelipa dola 2,500 kulipia kile cheti."

Spika aliwaeleza wabunge kuwa ni lazima waonyeshe mfano mzuri na hata kama serikali haijaomba kufanya uhakiki, uhalisia wa namna shahada zinavyotolewa wanaufahamu.

"Hizi nyingine zinazoleta wageni kwa ajili ya kuleta makabrasha ya vyeti vya kugawia watu wakiuza kama pipi haukubaliki, tunajivunjia heshima kama taifa hasa kwenye eneo letu la elimu na kuwapa heshima wanaostahili.

"Haya niliyosema hayazuii kuendelea na utaratibu wenu lakini mchukue jukumu la kufanya kama viongozi ambao kuna watu wanawaatazama nyuma na ninyi mna watoto wako shule na mngependa wasome mpaka wakutane na kibao kimegeuka," alisema.

Awali Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda akifafanua mwongozo wa mbunge huyo alisema zipo namna tatu za kupata PhD.

Alisema ya kwanza ni kwa kusoma darasani katika vyuo vinavyotambulika popote duniani, na ya pili ni kufanya utafiti baada ya kujisajili chuoni na nyingine ni ya heshima inayotunukiwa kwa mtu kutokana na mafanikio na michango yake. "Mfano Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), kina utaratibu wake ili mtu aweze kupewa, ni lazima kutolewe pendekezo ndani ya chuo na mtu anayetambulika, ufanyike utafiti na uhakikiwe," alisema.

# Kauli ya Mwigulu bungeni yazua jambo

**Na Romana Mallya,** DODOMA

KAULI aliyoitoa bungeni Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, wiki hii kuhusu uganga wa kienyeji, imeibua jambo na Spika kuagiza ifutwe katika kumbukumbu rasmi za Bunge (Hansard).

Mwigulu alisimama na kuomba mwongozo na kusema: 'hebu tujadili mambo mengine huko yanayohusu uganga wa kienyeji, ya uchumi tuyaache."

Kauli hiyo ilisababisha baadhi ya wajumbe kuchefukwa nayo na hata kumwomba Spika ifutwe.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akizungumza jana bungeni jijini hapa, alisema uamuzi uliochukuliwa ni kufuta maneno hayo katika taarifa rasmi za Bunge.

Aliyasema hayo wakati akitoa mwongozo ulioombwa na Dk. Mwigulu baada ya Mbunge wa Tandahimba, Ahmed Katani, kumtuhumu waziri kuwa amewatukana wabunge na kumtaka ajitafakari.

Spika alisema Februari7, mwaka huu, katika kikao cha sita cha mkutano wa 10 wa Bunge, alisimama Waziri Nchemba kuomba utaratibu chini ya Kanuni ya 75 na ya 71 za kudumu za Bunge.

"Mheshimiwa Mwigulu aliomba kuhusu utaratibu wakati Mheshimiwa Katani akitoa mchango wake katika taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) na taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kwa mwaka 2022.

"Katika mchango wake kama ulivyorekodiwa katika Taarifa Rasmi za Bunge, Mheshimiwa Katani alisema, namnukuu: 'Mimi ninawaambia fanyeni tathmini ya kina tunakwenda wapi? Kuna mambo unapaswa umwambie mtu mdogo sana. Mwigulu kaka yangu na rafiki yangu, umetutukana wabunge sana."

"Mimi ninakwambia umetutukana wabunge sana na unapaswa ukae na utafakari utakapokaa hapa. Hakuna anayeweza kujadili waganga wa kienyeji, hamna hamna.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya tunayojadili ni maisha ya Watanzania na tumeletwa bungeni tuwasaidie Watanzania," mwisho wa kunukuu.

Kutokana na kauli hiyo, Spika alisema Waziri Nchemba alisimama na kuomba utaratibu chini ya kanuni ya 75 na 71 na kueleza kuwa mbunge aliyekuwa anachangia amesema uongo.

Spika alinukuu maneno ya Waziri Nchemba aliyosema: "Mheshimiwa Naibu Spika kwa maslahi ya muda ninaomba mbunge anapochangia kanuni yetu inazuia kusema jambo la uongo, sasa Mheshimiwa mbunge anapo -generalize (kusema mambo ya ujumla) kwamba mimi nimewatukana wabunge.

"Hiyo ni allegation (madai) kubwa sana ambayo Bunge lako haliruhusu na mimi nisingeweza kutukana wabunge na kiti kikiwapo.'" mwisho wa nukuu.

Spika alisema kwa kuzingatia masharti ya kanuni ya 75 fasili ya Nne ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kiti kilitoa maelekezo kwa uamuzi kuhusu utaratibu ulioombwa kuwa utatolewa baadaye.

Alisema baada ya kuzipitia taarifa rasmi za Bunge, ametambua kwamba chimbuko la kauli ya Katani na baadhi ya wabunge wengine ambao wamekuwa wakizitoa bungeni kuhusu jambo hilo zinatokana na kauli ya Waziri Nchemba aliyoitoa Februari Mosi, mwaka huu, katika kikao cha pili cha mkutano wa 10.

Alisema Mwigulu alitoa kauli hiyo wakati akichangia taarifa ya kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii na taarifa ya kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

"Katika mchango wake, Mheshimiwa Mwigulu alitolea ufafanuzi hoja ya Mheshimiwa Luhaga Mpina alizokuwa amezibua wakati akichangia taarifa ya kamati hizo.

"Mheshimiwa Mwigulu alisema kama ifuatavyo ninanukuu: 'Mheshimiwa Mwenyekiti ninataka niweke kumbukumbu sawa. Katika baadhi ya mambo ili 'hansard' zako (taarifa rasmi za Bunge) ziweze kupata vizuri, nikianza na jambo moja ambalo ameliongelea Mheshimiwa Mpina.

"Katika mchango wake amechangia mengi lakini eneo mojawapo amesema tunapata mfumuko wa bei kwa sababu ya 'miss management' (kukosa usimamizi) wa sera za fedha. Akaelezea kwamba tumefanya malipo nje ya bajeti. Kwa maana hiyo, akakichukulia hicho kama kitu ambacho ni 'miss management' ya sera za fedha," alisema Mwigulu.

Spika alisema wakati Waziri Nchemba akimalizia, alisema; "'Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tujadili mambo mengine huko yanayohusu uganga wa kienyeji na vitu vingine kwenye uchumi,' this is my profession', tunajadilije hivi vitu ambavyo vipo clear.'"

Spika Tulia alisema kauli hiyo ndiyo iliyozua mtafaruku miongoni mwa wabunge na kuona wametukanwa ndiyo maana katika mchango wake, Katani akayatumia maneno hayo kwamba wabunge wametukanwa.

# Lissu afuata gari lake polisi aweke Makumbusho

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu amefika kwenye ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Martin Otieno akitaka kuliangalia gari lake aliloshambuliwa nalo kwa risasi mwaka 2017.

Lissu alifika jana kwenye ofisi hiyo na kupokewa na mmoja wa maofisa wa Jeshi la Polisi akidai kuwa aliwasiliana na kamanda ili kuangalia gari lake kwa kuwa hajawahi kuliona.

Hata hivyo, Lissu alidai kutomkuta Kamanda Otieno ofisini kwa kuwa alikwenda kwenye tukio la ajali ya basi kugongana na lori huko Kongwa mkoani Dodoma.

Alimwomba ofisa wa polisi aliyekuwa akizungumza naye kuliona gari lake lakini alimwambia ni vyema amsubiri Kamanda Otieno kwa kuwa waliwasiliana.

Akizungumza baada ya kutoka ofisi hiyo, Lissu alisema aliwasiliana na kamanda huyo asubuhi akitokea Singida namna ya kupata gari lake.

"Tangu septemba 7, 2017 gari lile limekuwa mikononi mwa polisi na sijawahi kuliona, nilikuja kuliona lilivyoharibiwa ili kuona namna ya kulitumia gari langu kwa kuwa ninahitaji kulitumia au kupeleka Makumbusho," alisema.

Aliahidi kumsubiri kamanda na atazungumza naye akimaliza jukumu lililompeleka Kongwa.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Manajimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi (kushoto), akikabidhi tuzo kwa Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, CPA, Hosea Kashimba, jijini Arusha jana, kwa ajili ya kufanikisha sherehe za miaka kumi ya e-GA na kikao kazi cha tatu cha serikali mtandao. Kulia ni Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk.Laurean Ndumbarona Mkurugenzi Mkuu wa e-GA, Mhandisi Benedict Ndomba. Habari uk. 7. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Muswada kufumua sheria ya Habari kusomwa leo

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

MUSWADA wa Marekebisho ya Sheria ya Huduma ya Habari, 2016 unatarajiwa kusomwa leo bungeni jijini hapa kwa mara ya kwanza.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye alibainisha hayo jana jijini hapa alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu mchakato wa muswada huo kupelekwa bungeni.

Alisema serikali imepambana kuhakikisha muswada huo unapata nafasi ya kusomwa kwa mara ya kwanza katika Bunge hili.

"Tumepambana lakini Bunge hili lilikuwa kwa ajili ya kupokea taarifa za kamati za kudumu za Bunge na kutokana na majadiliano marefu kati yetu na Bunge tulielezwa kuwa haitawezekana muswada huu kusomwa katika Bunge hili," alisema Nnauye

Alisema muswada uliokuwa umepangwa kusomwa katika mkutano huu wa Bunge ni wa Bima ya Afya kwa Wote.

"Na huu wa kwetu, Spika alitangaza kuwa usubiri hadi Bunge lingine na mimi nilipokutana na waandishi wa habari hivi karibuni niliwapatia mrejesho kuwa muswada huu hautasomwa katika Bunge hili lakini leo wakati tukiendelea kupambania nafasi hii tumepata taarifa kuwa Spika ametupatia fursa ya muswada huu kusomwa bungeni kwa mara ya kwanza kesho (leo)," alisema Nape.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha muswada huo unakwenda na kufika kule ambako walikuwa wanatarajia na siyo vinginevyo.

"Kuna watu badala ya kutafuta ufafanuzi lakini wao wanatoa 'statement' (tamko) ya jumlajumla kuwa serikali inapiga danadana kwenye mchakato huu.

"Kama kuna jambo serikali tunalisukuma usiku na mchana ni kuhakikisha kuwa hili jambo linaisha na mie nimetoa muda wangu mwenyewe binafsi wa kukutana na wadau kuzungumza, kusukuma, kutoa taarifa na kila mara nimekuwa nikitoa taarifa, hili limenisikitisha sana," alisema.

Nape alisema taarifa iliyotolewa na Jukwaa la Wahariri (TEF) juzi inaonyesha kana kwamba serikali imegawanyika vipandevipande, jambo ambalo siyo sahihi.

"Ninashindwa kuelewa lengo la kauli ile ilikuwa nini au kuichonganisha serikali na wanahabari, ninataka niwathibitishie Watanzania na waandishi wa habari kuwa serikali yetu ni kitu kimoja.

"Sheria hii ni ya wanahabari wote, ninataka tuendelee kuwa na imani na serikali ina nia njema ya kuhakikisha kwamba hii sheria inapitiwa na inafika pale ambapo tumekubaliana,"" alisema. Aliwataka waandishi wa habari kuendelea kuwa na imani na mchakato huo kuwa utakwenda na utaisha salama.

"Tumefanya mengi pamoja kwa ushirikiano na siyo kwenda kukimbilia kusema hadharani, tuendelee kutumia njia hiyohiyo ya ushirikiano kuliko kunyoosheana kidole kwani Rais ndiye aliyetoa maelekezo kwamba jambo hili liende," alisema Nape aliyeonyesha wazi kukerwa na tamko la TEF la juzi kuhusu mchakato wa marekebisho ya sheria hiyo.

## Mshtakiwa alia kusota miaka 8 kesi ya bangi

**Na Grace Gurisha**

MSHITAKIWA Hassan Banda anayedaiwa kukutwa na bangi, ameiomba mahakama arudishwe katika kituo cha polisi hadi pale upelelezi utakapokamilika, kwa sababu mpaka sasa yuko gerezani kwa kile kinachodaiwa upelelezi haujakamilika.

Aidha, amedai kuwa hivi karibuni, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan alitaka kesi zisizokuwa na msingi zifutwe kwa sababu kesi yake hadi sasa imefutwa mara tano na kufunguliwa upya kwa madai kwamba upelelezi bado.

Banda alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Evodia Kyaruzi, wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya kutajwa. Wakili wa Serikali, Monica Ndakidemi, alidai kuwa upelelezi haujakamilika.

Alidai kuwa faili bado liko kituo cha polisi na kwamba limerudishwa kwa ajili ya marekebisho ya kiupelelezi, hivyo akaomba tarehe ya kutajwa.

"Kesi yangu ina mwaka wa nane tangu Agosti, 2016 nilipokamatwa. Kila siku majibu ni yale yale ya upande wa mashtaka kuwa upelelezi bado haujakamilika.

"Nimekaa gerezani muda mrefu hadi naumwa mgongo, macho na pumu. Pia niliandika barua ya kuingia makubaliano 'plea bargaining' lakini sijapata. Nimechoka kukaa gerezani, naomba mahakama inirudishe polisi hadi upelelezi utakapokamilika ndiyo niletwe mahakamani," alidai.

Pia alidai kuwa kesi yake imeshafutwa mara tano na kufunguliwa upya kwa mashtaka yale yale huku familia na ndugu wakiwa wanamtegemea, hivyo akaomba aonane na kiongozi wa waendesha mashtaka mahakamani hapa, Grace Mwanga, ili amsaidie.

Baada ya mshtakiwa huyo kudai hayo, Hakimu Kyaruzi alisema hoja zilizotolewa ni za msingi kwa hiyo tarehe ijayo kama upande wa mashtaka hautakuwa na jibu la kuridhisha mahakama itamruhusu aonane na Mwanga.

Akijibu hoja za mshtakiwa, Wakili Ndakidemi alidai kuwa alichokidai ni cha kweli, kwa hiyo atajitahidi kuwasiliana na uongozi wa polisi ili kurudisha faili kesi iendelee.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Februari 21 kwa ajili ya kutajwa na kuangalia hatua za faili zilipofikia.

Inadaiwa kuwa Agosti 25, 2016 mshtakiwa akiwa eneo la Mbezi Kibanda cha Mkaa wilayani Ubungo, alikutwa na bangi.

## HABARI KITAIFA

# Majaliwa ataja mkakati wa serikali kudhibiti ubadhirifu fedha za umma

**Na Romana Mallya,**
DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema katika kukabiliana na vitendo vya ubadhirifu wa mali na fedha za umma, serikali imeanzisha na kukiboresha kitengo cha ufuatiliaji na tathmini na sasa kinapita mamlaka ya serikali za mitaa na taasisi za umma kuona yanayoendelea.

Siku tatu zilizopita, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) wakati ikiwasilisha taarifa yake bungeni, ilionyesha madudu katika halmashauri tatu za manispaa na moja ya wilaya, ikiwamo fedha zilizoingizwa benki na kutoka siku moja, miamala kufutwa au baadhi ya tarakimu kurekebishwa bila idhini ya maofisa masuhuli.

Jana, wakati wa maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu, Mbunge wa Arumeru Magharibi, Noah Saputu, alisema mara kwa mara wamekuwa wakiona jitihada za Waziri Mkuu za kuzunguka nchini kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema katika ziara hizo amekuwa akikuta baadhi ya miradi haitekelezwi vizuri na kuwapo kwa ubadhirifu, wizi na uzembe wa aina mbalimbali huku ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ikiibua ubadhirifu.

Kutokana na hali hiyo, mbunge huyo alitaka kujua upi mkakati wa makusudi na maalum ambao serikali inachukua kuhakikisha wizi na ubadhirifu kwenye miradi ya umma hautokei.

Akijibu swali hilo, Majaliwa alisema serikali ina mfumo wa kufanya tathmini kwenye sekta mbalimbali ikiwamo kufanya mapitio ya mwenendo na matumizi ya fedha na mali za umma.

“CAG ni taasisi mojawapo ambayo inakwenda kuona mwenendo namna mali na fedha za umma kwenye sekta zote za serikali na ikibidi pia, sekta binafsi ambayo ina maslahi ya moja kwa moja kwa serikali.

“Upo ukweli kwamba wanapofanya kazi hiyo, wanabaini mapungufu na wakati mwingine mapungufu hayo wachache wanafanya kwa makusudi na CAG anachokifanya ni kuishauri serikali namna bora ya kudhibiti hali hiyo kwenye maeneo hayo,” alisema.

Majaliwa alisema ni kweli alipata nafasi ya kufanya ziara kwenye halmashauri, taasisi mbalimbali za serikali na anapokwenda wakati mwingine huenda na taarifa ya CAG ambayo inashauri serikali, namna bora ya kusimamia maeneo hayo na kuchukua hatua.

“Namna gani nzuri ya kuendelea kusimamia, kwanza tunatambua mchango wa taasisi hii ambao pia unatuainishia na kubainisha mapungufu hayo kwenye sekta za serikali.

“Kazi yake ya kushauri serikali tunaichukua na kuifanyia kazi, pale tunapoona ubadhirifu wa moja kwa moja tunachukua hatua, pale ambako anashauri namna bora ya kuboresha tunafanya hivyo, na sasa serikali imeandaa mfumo mzuri sana wa kufuatilia sekta zetu kabla CAG hajafika,” alisema.

Alisema ofisi yake imeanzisha kitengo cha ufuatiliaji na tathmini kwenye sekta za serikali ambazo zinabaini mapungufu hayo kabla CAG hajafika.

“Na kitengo hiki tumekiimarisha zaidi na kimeshaanza kazi, sasa hivi kinapita kwenye mamlaka za serikali za mitaa, taasisi mbalimbali za serikali, ili kuona hali hiyo na kufanya tathmini na pia kushauri pale kwenye mapungufu kwenye sekta hiyo kabla CAG hajafika.

# Mtandao watoa hoja nane kutokomeza ukeketaji

**Na Sabato Kasika**

MTANDAO wa Kupinga Ukeketaji Tanzania, umetoa mapendekezo manane yatakayosaidia kutokomeza mila potofu zinazochangia kuendelea kwa vitendo vya ukeketaji nchini.

Akisoma mapendekezo hayo mbele ya waandishi wa habari juzi jijini Dar es Salaam, Mratibu wa Mtandao huo, Getrude Dyabene, alisema mbali na jitihada zinazofanywa na serikali na wadau wake katika kutokomeza vitendo hivyo, bado kuna mambo ya kufanya ili kuondoa mila hiyo potofu.

Dyabene alisema mtandao unapendekeza kutungwa na kupitisha sheria ya kuzuia ukeketaji, kurekebisha Sheria ya Mtoto na Kanuni ya Adhabu ili kuongeza adhabu katika makosa ya ukeketaji kwenye kifungu cha faini. “Katika pendekezo hili la kwanza, tunashauri pia maboresho ya sheria yajumuishe na kuweka makosa ya wazee wa mila na wazazi wanaojihusisha na ukeketaji,” alisema Dyabene.

Alitaja pendekezo lingine kuwa ni kutaka viongozi wa ngazi za juu kujitokeza wazi wazi na kuunga mkono jitihada zinazoendelea za kutokomeza vitendo vya ukeketaji.

“Lakini pia katika pendekezo letu la tatu, ni kutaka serikali kupitia wizara za kisekta kutenga bajeti ya utekelezaji wa mpango kazi wa kitaifa wa kutokomeza ukeketaji wa mwaka 2021 hadi 2024,” alibainisha.

La nne kuwa ni kuitaka serikali kutekeleza kwa vitendo mpango kazi wa kikanda wa nchi tano kuhusu ukeketaji unaovuka mipaka, huku pendekezo la tano, likiwa ni serikali kusimamia kikamilifu sheria, ili wakeketaji wakamatwe na kuwajibishwa kwa mujibu wa sheria za nchi.

“Pendekezo letu la sita, tunaishauri serikali kudumisha ushirikiano na taasisi zisizo za kiserikali na mashirika rafiki ya kimataifa, ili kwa pamoja tutokomeze ukeketaji na ukandamizaji kwa watoto wa kike na wanawake,” alisema.

Mtandao huo katika pendekezo la saba, unaishauri jamii kuungana na kukemea ukeketaji, kushirikiana na vyombo vya dola, ikiwamo kutoa taarifa na ushahidi, ili kufanikisha vita dhidi ya ukatili wa kijinsia kwa ujumla.

Dyabene ambaye pia ni Ofisa Mwandamizi wa Jinsia, Wanawake, Watoto na Watu Wenye Ulemavu kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), alitaja pendekezo la nane kuwa ni kuwataka wadau kuongeza juhudi katika kuifikia jamii inayotekeleza mila ya ukeketaji na kuipa elimu ili ibadilike.


twiga cement
HEIDELBERGCEMENT Group

## UNAUDITED RESULTS
FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2022

**CHAIRMAN'S STATEMENT**
Tanzania Portland Cement Public Limited Company (TPCPLC) continues to deliver strong operating results when compared to year 2021. Both the sales volume and revenue reached a record high compared to year 2021. Sales volume and revenue increased by 5% and 10% respectively. This increase is due to the continued increased demand of cement products within Tanzania and outside Tanzania.

The high availability and efficiency of the plant and machinery has contributed to the improved performance compared to year 2021, all within an environment where the Health and Safety of our employees and contractors is paramount. The Company continues to focus on delivering excellent customer service, selling of high quality products and maintaining strong customer relationships to enable TPCPLC to demonstrate its strength as the leading player in the industry.

| INCOME STATEMENT | JAN - DEC 2022 TZS'000 | JAN - DEC 2021 TZS'000 |
|---|---|---|
| Revenue | 494,716,182 | 449,509,302 |
| Cost of sales | (311,469,289) | (277,156,918) |
| **Gross profit** | **183,246,893** | **172,352,384** |
| Other operating income | 1,851,771 | 2,155,770 |
| Selling and administrative expenses | (2,742,758) | (2,589,758) |
| Administrative expenses | (21,449,364) | (19,751,617) |
| Depreciation and amortisation | (20,645,405) | (19,647,478) |
| Other operating expenses | (2,918,648) | (5,352,943) |
| **Operating profit** | **137,342,489** | **127,166,358** |
| Financial items | 2,755,079 | 870,830 |
| **Profit before tax** | **140,097,568** | **128,037,188** |
| Taxes on income | (42,738,361) | (39,555,603) |
| **Profit for the year** | **97,359,207** | **88,481,585** |

| BALANCE SHEET | 2022 TZS'000 | 2021 TZS'000 |
|---|---|---|
| **ASSETS** | | |
| Intangible fixed assets | 813,318 | 1,006,537 |
| Tangible fixed assets | 143,311,095 | 145,850,876 |
| Right of use assets | 574,000 | 982,483 |
| Other non-current assets | 4,333,992 | 796,000 |
| **Non.current assets** | **149,032,405** | **148,635,896** |
| Inventories | 85,992,839 | 52,935,487 |
| Trade and other receivables | 76,095,754 | 62,864,186 |
| Other non-current assets | 600,000 | 600,000 |
| Cash and cash equivalents | 105,512,644 | 114,278,364 |
| **Current assets** | **268,201,237** | **230,678,037** |
| **TOTAL ASSETS** | **417,233,642** | **379,313,933** |
| **EQUITY & LIABILITIES** | | |
| **Equity** | **299,739,076** | **272,235,501** |
| Lease liabilities | 1,149,572 | 186,758 |
| Long term provisions | 9,605,633 | 7,739,484 |
| Provision for deferred taxes | 10,066,670 | 11,618,859 |
| **Non-current liabilities** | **20,821,875** | **19,545,101** |
| Lease liabilities | 3,461,375 | 1,044,405 |
| Current income tax payable | 521,083 | 28,859 |
| Trade and other payables | 89,784,862 | 83,611,599 |
| Dividend payable | 2,905,373 | 2,848,468 |
| **Current liabilities** | **96,672,693** | **87,533,331** |
| **TOTAL EQUITY & LIABILITIES** | **417,233,642** | **379,313,933** |

**Prospects**
The cement demand in Tanzania and in the East-African region has been growing steadily in recent years. TPCPLC is well placed to meet this growing demand and will continue to work on improving efficiency and operating performance.

**Appreciation**
The Board would like to thank all its stakeholders for their support. We have every confidence that TPCPLC will continue to deliver value for the shareholders and community in the future.

BY ORDER OF THE BOARD

Hakan Gurdal
Chairman of the Board
06.02.2023

**Tanzania Portland Cement Public Limited Company**
**P.O.Box 1950**
**Dar-es-salaam**
**Tanzania**
**www.twigacement.co.tz**
**Email: info@twigacement.co.tz**

217273802

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bunge lisifanywe sehemu ya mipasho, na kuibua utengano

**MKUTANO** wa 10 wa Bunge unatarajiwa kumalizika leo jijini Dodoma baada ya kufanyika kwa takriban wiki mbili. Katika mkutano huo, kuna mambo mengi yaliyofanyika yakiwamo maswali ya kawaida, maswali kwa Waziri Mkuu na taarifa za kamati za kudumu za bunge.

Baadhi ya taarifa za kamati husussan ile ya Hesabu za Serikali za Mitaa, yaliibuliwa madudu yaliyofanywa na baadhi ya halmashauri hali iliyoonyesha kuwa bado kuna ubadhirifu na ufisadi wa kutisha katika mamlaka hizo zilizopewa jukumu la kutekeleza moja kwa moja miradi ya maendeleo ya sekta mbalimbali zikiwamo elimu, afya, maji, kilimo na miundombinu.

Hatua hiyo imesababisha baadhi ya wabunge kuja juu na kuchukua hatua dhidi ya waliohusika ikiwamo kuchukuliwa hatua za kisheria badala ya kuwahamisha kutoka halmashauri moja kwenda nyingine, jambo ambalo limezoeleka.

Kuwapo kwa madudu hayo si jambo geni kwani kila kamati zinapowasilisha ripoti zao, yamekuwa yakianikwa sambamba na ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Pamoja na hayo ambayo ni kawaida kutokea kila mara, jambo kubwa ambalo limeibua mijadala ni kauli za baadhi ya wabunge na mawaziri walizozitoa wakati wa kuchangia taarifa mbalimbali na kujibu hoja zilizotolewa wakati wa mijadala.

Moja ya mambo hayo ni kauli ya mbunge mmoja kulalamikia mfumo wa ajira katika utumishi wa umma na taasisi za serikali kuwa si rafiki, hivyo kushauri kwamba utaratibu wa sasa ubadilishwe na badala yake ufanyike kikanda!

Mbunge huyo bila kutafakari nini anachokisema na kwa mustakabali wa maslahi mapana ya taifa, alisema serikali itoe ajira kwa kigezo cha wilaya, mikoa au majimbo, ili vijana walioko katika maeneo hayo wanufaike!

Licha ya kauli hiyo, Waziri wa Fedha na Mipango, alikabwa koo na baadhi ya wabunge pale aliposema watu waache kujadili masuala ya uchumi ambayo ni taaluma yake badala yake wakajadili masuala ya uganga wa kienyeji.

Hata hivyo, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, jana alitoa ufafanuzi baada ya kuombwa mwongozo na baadhi ya wabunge na kuona majibu hayo ya Waziri hayakuwa ya staha, hivyo kuyafuta katika kumbukumbu rasmi za bunge.

Wabunge ni watu wenye hadhi ya hali ya juu na jamii inaamini kwamba kwa kupata nafasi hiyo, wanapaswa kuzingatia miiko na maadili pamoja na tunu za taifa ambazo pamoja na mambo mengine ni uhuru, umoja na mshikamano.

Jambo la kujiuliza ni je, kuna ulazima mtu mwenye heshima kama mbunge akasimama na kuhubiri habari za umajimbo kwa madai kwamba ajira kwa vijana katika serikali zitolewe kwa misingi hiyo? Kwa zaidi ya miaka 60 tangu nchi ipate uhuru bado kuna watu wanaendelea kuhubiri habari za umajimbo na umikoa kwa maana keki ya taifa igawanywe kwa misingi hiyo?

Hata majibu yaliyotolewa na waziri na hatimaye kuibua mijadala kila kona ikiwamo mitandao ya jamii, hayakuwa ya kistaarabu hata kidogo ndiyo maana Bunge limeamua kuyafuta kwenye kumbukumbu rasmi (Hansard).

Ni vyema wabunge, ambao ni wawakilishi wa wananchi, wakiwamo mawaziri, wakalitumia Bunge wakati wa mikutano yake, kuzungumza kauli zenye staha na kujiepusha na mambo ambayo yanaweza kuwa na sura na mitazamo ya kibaguzi. Kwa maneno mengine, Bunge lisifanywe kama kijiwe cha kujipatia umaarufu au mipasho.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Ni vyema ujenzi barabara ya Musoma hadi Suguti ukamilike kwa wakati

Na Sabato Kasika

**MRAD**I wa ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita tano kutoka kijiji cha Kusenyi hadi Suguti, wilayani Musoma mkoa wa Mara, ulianza Julai mwaka 2019, kwa matarajio kumalizika siku kama hiyo mwaka unaofuata.

Hata hivyo, muda wa mkataba uliongezwa hadi kufikia Aprili 2022, ili ujenzi uwe umekamilika, lakini hadi kufika Januari mwaka huu, mkandarasi bado alikuwa anaendelea na ujenzi.

Nadhani, tunaendelea kuchelewa. Ukamilishaji wa mradi huo unaweza kuchangia kukwamisha shughuli za kiuchumi za Musoma Vijijini, zikiwamo biashara zao maarufu samaki, madini na mazao ya biashara.

Kama kipande cha kilomita tano kimejengwa kwa miaka hiyo yote na bado hakijakamilika. Najiuliza je, hizo kilomita 92 zitachukua miaka mingapi kukamilika?

Ni vyema sasa, ujenzi huo ukafuatiliwa ili kujua tatizo liko wapi. Pamoja na kwamba, kilomita tano ni ndogo, lakini zinasaidia kupunguza kero ya barabarani, hasa wakati wa mvua ikiwawezesha wananchi kusafirisha mazao yao kirahisi.

Kuchelewa kukamilishwa kipande hicho kilomita chache, kunaashiria rehani ya hizo kilomita nyingine 87 zilizobaki kwenye mradi, pale ujenzi awamu ya pili utakapoanza.

Niseme, kiuchumi eneo hilo linapaswa kutazamwa kwa jicho la ziada, kuhakikisha barabara inajengwa yote kwa kiwango cha lami, tena kwa wakati, ili wananchi wanufaike ipasavyo.

Mnamo Machi Mosi mwaka jana, Wajumbe wa Bodi ya Barabara Mkoa waliutembelea mradi huo, mkuu wa kampuni inayojenga barabara, akajitetea kwa ufafanuzi mradi huo unatekelezwa kwa kasi.

**Niseme, kiuchumi eneo hilo linapaswa kutazamwa kwa jicho la ziada, kuhakikisha barabara inajengwa yote kwa kiwango cha lami, tena kwa wakati, ili wananchi wanufaike ipasavyo.**

Akawaambia wajumbe hao kuwa, ili kuhakikisha mradi unakamilika, yapo mambo kadhaa yaliyofanywa na kampuni yake, ikiwamo kufunga mtambo wa kusaga kokoto wenye uwezo wa kusaga tani 200 kwa saa.

Pia, akataja mambo mengi waliyokuwa wameyafanya kuwa ni ujenzi wa tuta lenye ujazo wa mita za ujazo 430,000, kusambaza tabaka la kwanza kisha la pili ili baadaye kuwekwa lami na kuahidi kazi ingekamilika ndani ya siku 60 zilizobakia.

Pia, akataja sababu zinazoufanya mradi kutekelezwa kwa kasi ndogo, ni kutopatikana fedha, mkataba wa kazi, huku akifafanua kuwa utekelezaji wa mradi ni wa kuridhisha kulingana na hali halisi, ingawa hakutoa ufafanuzi zaidi. Maelezo hayo yalimfanya aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mara wakati huo, Ally Hapi, kumuagiza mkandarasi huyo kumaliza mradi kwa wakati, akikumbusha asimame kwenye takwa la mkataba wake.

Pamoja na kutumia miaka hiyo yote bila kukamilika, kuna malalamiko kutoka kwetu wakazi wa vijiji jirani kama vya Kusenyi na Suguti.

Binafsi nahisi dalili za ufanisi kwenye mradi huo wa barabara ya lami kusuasua njia panda, nikilalamikia uende kwa ufansi wa kimkataba, kwa wakati na hata ubora. Ni ushauri, wenye mamlaka kutafutia majibu sahihi.

Sisi wakazi tunaamini hilo la kutokamilika barabara, haliishii tu katika kutukwamisha kihuduma, bali inagusa maisha yetu kwa undani na ndiyo maana tunaona haja kwa wataalam wa mradi huo kuwajibika zaidi na uongozi wao hata mradi uwe na tija, pia manufaa kwetu sote na ndiyo inavyojengwa.

# Wahandisi GGML wazuru Daraja Kigongo-Busisi

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

KUNDI la wahandisi 40 kutoka Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) limetembelea Daraja la Kigongo-Busisi linalounganisha mikoa ya Mwanza na Geita kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu kuhusu mambo mapya yanayogusa sayansi, teknolojia na uvumbuzi unaotumika duniani kwenye sekta ya ujenzi.

Ziara hiyo ambayo ni sehemu ya mipango ya Kampuni ya GGML kuendeleza wafanyakazi wake kupitia ziara mbalimbali za kimafunzo kwenye miradi mikubwa ya kihandisi ilifanyika juzi.

Akitoa maelezo kwa wahandishi hao kutoka GGML, Mhandisi Abdukarim Majuto kutoka kundi la Kampuni za Ushauri wa mradi wa ujenzi wa daraja hilo, alisema mradi huo umetumia teknolojia ya hali ya juu inayotumiwa na wahandisi duniani kote.

Alisema teknolojia inayotumika katika ujenzi wa miradi mikubwa chini ya maji ni moja ya kivutio cha kutembelea eneo la Daraja la Kigongo-Busisi.

"Daraja lina urefu wa kilometa 3.2 katika Ghuba ya Mwanza na kuunganisha Kigongo mkoani Mwanza na Busisi mkoani Geita, ni moja ya maeneo ya kuvutia zaidi nchini," alisema.

Ziara hiyo ilihusisha vikundi vya mafundi wakiwamo wahandisi wa mitambo, umeme na viwanda, wasimamizi wa miradi, mafundi mekanika na wataalamu wa kuchomelea vyuma.

Meneja wa Miundombinu wa GGML, Eliakim Kagimbo alisema kampuni yao inalitumia daraja hilo kama jukwaa la kujifunzia ili kupata maarifa ya kina juu ya vipengele vya kiufundi vya mradi mzima.

"Tuna furaha kuona daraja hili linajengwa karibu na tunakofanyia shughuli zetu. Kama unavyojua, GGML imetekeleza miradi kadhaa ya uhandisi kwa miaka mingi na daraja hili linatoa fursa kwetu kuboresha ujuzi wetu," alisema.

Msimamizi wa Ujenzi wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROAD) kwenye daraja hilo, William Sanga alisema ziara hiyo ya mafunzo ni muhimu katika utekelezaji wa programu ya maendeleo ya nchi.

"Daraja la Kigongo-Busisi litakuwa kiungo muhimu kati ya Mwanza na mikoa ya jirani pamoja na nchi jirani. Kwa hiyo, lina uwezo wa kuchochea ukuaji wa uchumi kwenye eneo hili.

"Daraja hili litapunguza kwa kiasi kikubwa cha foleni kwenye njia hii na pia kuboresha usalama wa watumiaji katika kivuko cha ziwa hili," alisema.

Tangu kuanzishwa kwake, GGML imekuwa ikifanya kazi kwa karibu na mamlaka za serikali za mitaa kusaidia miradi kadhaa ya jamii katika Mkoa wa Geita kupitia ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi pamoja na programu za kitaifa.



Mhandisi Abdukarim Majuto (kushoto) kutoka kundi la Makampuni ya Ushauri wa mradi wa ujenzi wa daraja la Kigongo – Busisi, akitoa maelezo ya mradi huo, kwa wahandisi na watalaam mbalimbali kutoka GGML, walipotembelea hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Matumizi ya TEHAMA PSSSF yamkuna waziri

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

NAIBU Waziri ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi amezipongeza taasisi za umma, ukiwamo Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) kwa kuwafikia wananchi kiurahisi kwa kutumia matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Ndejembi alipongeza hatua hiyo jijini hapa jana kupitia hotuba yake ya ufunguzi sherehe za kutimiza miaka 10 ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) na kikao kazi cha tatu cha Serikali Mtandao kinachokutanisha wataalamu wa TEHAMA kutoka serikalini.

"Leo (jana) nimejionea kwenye mabanda pale PSSSF wameweza kuweka App ili kuona michango inavyokwenda, hivyo nielekeze e-GA kuendelea kufanya utafiti ili kuleta ubunifu wa mifumo ya TEHAMA itakayoliwezesha taifa kufanikiwa kuimarisha sekta za viwanda, biashara na uwekezaji na kulipeleka mbele taifa letu kimaendeleo.

"Na katika hili nitoe pongezi pia kwa taasisi ambazo tayari zimeweza kuwafikia wananchi kiurahisi zaidi na kuondoa urasimu wa makaratasi," alipongeza.

Ndejembi alizishauri taasisi zingine za umma kutumia TEHAMA ili kuwarahisishia wananchi kupata huduma za serikali kwa haraka.

PSSSF ina huduma za PSSSF Kiganjani na PSSSF Mtandaoni. Huduma hizi ni suluhisho kwa wanachama, wastaafu na waajiri kupata huduma popote walipo na muda wowote kwa kutumia simu janja au kompyuta bila kuhitaji kufika kwenye ofisi za PSSSF.




# WE ARE HIRING
## "TANZANIAN NATIONALS"

**Location: Tanzania**

**Job Opening for:**

- Senior Planning Engineer Local
- Draftsman Local
- Doc controller Local
- IT Engineer Local
- Purchaser Expeditor / Dar
- Purchaser Expeditor / Tanga
- Local Liason Officer
- Cost & Report Engineer
- Quantity Surveyor Local
- QA/QC officer I Local
- QA/QC Inspector Local
- QA/QC Inspector Assistant Local
- QA/QC Inspector Assistant Local
- QA/QC Inspector Assistant Local
- Inspector
- Enviromental Inspector
- Site Nurse
- Security Commandor
- Watch Commandor
- Site Accountant/Payroll Local
- Welding Supervisor Local
- Welding Supervisor Local
- Trestle - Site Engineer Local
- Deep Trestle Supervisors Local
- Deep Trestle Supervisors Local night
- Pile weld foreman
- Pile weld foreman night
- Trestle - Site Engineer Local
- Trestle - Site Engineer Local
- head Concrete Supervisor
- head Concrete Foreman
- Precast yard superintendent
- Precast yard engineer
- Precast yard foreman
- Precast yard QA/QC Inspector
- MEP HSE Safety Coordinator
- Plant Mechanic Local
- Site Electrician
- Assistant Surveyors
- Logistics Foreman Local
- Construction QC Advisor - Coating
- Construction QC Advisor LLHT
- Construction QC Advisor HV/LV
- Construction QC Advisor - Welding / NDE
- Civil QC Supervisor
- Company Site Representative (Construction)
- Human Resources and Administrative Specialist.
- HSE Expert/ Consultant

All candidates must have a minimum of 5 years of experience and must perfectly be fluent in English, Swahili both Written and Spoken



**Apply Now at : isubmit.cv.tz@gmail.com**

21727202

# Uzalishaji mafuta alizeti sasa tani 300,00

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa tathmini ya mwaka 2020/21, inaonyesha uzalishaji wa ndani wa mafuta ya alizeti ni asilimia 75 ya kiasi cha wastani wa tani 300,000 za mafuta ya kula yanayozalishwa nchini kwa mwaka.

Mikoa inayozalisha alizeti kwa wingi ni Singida, Dodoma, Manyara, Shinyanga, Iringa, Tabora, Morogoro, Ruvuma, Mbeya, Arusha, Lindi, Mtwara, Rukwa na Mara.

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Chumbuni (CCM), Ussi Salum Pondeza.

Mbunge huyo alihoji ni kwa nini serikali isiongeze uzalishaji wa mafuta ya alizeti nchini kwa ajili ya soko la Zanzibar na Bara kuliko kuagiza mafuta hayo kutoka nje ya nchi.

"Je, hali ya uzalishaji wa mafuta ya alizeti ikoje kwa mwaka na ni mikoa gani inayozalisha zaidi Tanzania Bara?"alihoji.

Akijibu maswali hayo, Mavunde alisema serikali inatekeleza mkakati wa kuongeza uzalishaji wa mazao ya mafuta nchini, kwa lengo la kupunguza uagizaji wa mafuta ya kula na kuongeza uzalishaji kutoka wastani wa tani 700,000 hadi tani milioni 1.5 ifikapo mwaka 2025.

"Utekelezaji wa mpango huo unajumuisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kwenye mashamba ya mbegu ya Wakala wa Mbegu za Kilimo na kwa mwaka 2022/23 Sh. bilioni 43.03 zitatumika kwa lengo hilo,"alisema.

Hata hivyo, alisema mahitaji ya mafuta ya kula nchini ni tani 650,000 kwa mwaka.

Akiuliza swali la nyongeza, Mbunge huyo alihoji kauli ya serikali ya kufidia wakulima waliopata hasara kwenye mbegu za alizeti zilizokuwa zikitolewa na Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA).

Mavunde akijibu swali hilo, alikiri msimu uliopita wakala huo ulisambaza mbegu za alizeti kwenye baadhi ya maeneo zilifanya vizuri na maeneo mengine hazikufanya vizuri.

"Ziko sababu zilizofanya kutofanya vizuri kutokana na misimu ya kupanda na changamoto zingine za mabadiliko ya tabianchi, katika kutatua changamoto hii kwa mwaka 2022/23 serikali imetenga fedha ili kugawa mbegu za ruzuku kwa wakulima ambapo kilo mbili atapata kwa Sh.10,000 ili kuondokana na changamoto waliyopata,"alisema.

Aidha, alisema kuanzia hivi sasa ASA imepewa maelekezo ya kuanza kuzalisha mbegu zenye



Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Kilosa ambaye amehamishiwa Wilaya ya Mlele, mkoani Katavi, Majid Mwanga (kushoto), akimkabidhi ofisi Mkuu mpya wa Wilaya hiyo, mkoani Morogoro, Shaka Hamdu Shaka, mjini Kilosa mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Afrika yapewa mbinu kumaliza tatizo la maji

**Na Mwandishi Wetu**

UWEKEZAJI katika upatikanaji wa maji ya chini ya ardhi, umetajwa kuwa ni mbinu ambayo inaweza kusaidia kukabiliana na ukosefu wa huduma hiyo muhimu kwenye maeneo ya mijini na vijijini Afrika, Tanzania ikiwamo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Davis & Shirtliff Tanzania, Benjamin Munyao, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema sehemu nyingi barani Afrika zimekuwa zikikabiliwa na upatikanaji wa maji kutokana na sababu mbalimbali, zikiwamo mabadiliko ya tabianchi na ukosefu wa mvua za kutosha.

"Hivyo ni bora uwezekazaji kwa ajili ya utafutaji wa maji chini ya ardhi ukafanyika ili kukabiliana na changamoto hiyo," alisema Munyao.

Alisema upatikanaji wa maji yanayotoka ardhini, unahitaji uboreshaji wa mifumo ya uendeshaji, uwekezaji katika miundombinu, uwezeshaji wa rasilimali watu na ushirikiano wa wadau muhimu katika sekta ya maji na kuwa na mifumo ya udhibiti wa upotevu wa huduma hiyo muhimu.

Mkurugenzi huyo wa kampuni ya kusambaza vifaa vinavyosaidia upatikanaji maji na nishati katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini, alisema Tanzania na nchi zingine barani Afrika zinakabiliwa na ongezeko la upotevu wa maji ya ardhini kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu na kupungua kwa rasilimali hiyo kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa.

"Nchi kama Tanzania kwa mfano inahitaji kuweka viwango vya ubora wa maji yanayopatikana kutoka chini ya ardhi na kuweka mifumo ya kuruhusu upimaji wa ubora huo mara kwa mara. Lakini pia inahitaji kuendelea kufanya utafiti wa ubora wa maji hayo yanayopatikana kutoka ardhini ili kujua ubora wake," alisema.

Alitoa wito wa kuimarishwa kwa miundombinu na kuongeza uwekezaji katika ufuatiliaji wa maji chini ya ardhi ili kukidhi mahitaji ya upatikanaji wa maji safi na salama.

Pia alishauri uwekezaji zaidi katika uchimbaji wa visima na kutumia vitambuzi na teknolojia zinazoweza kutumika kufuatilia rasilimali za maji chini ya ardhi katika kupata na kukusanya data muhimu kwa ajili ya utabiri bora utakaokabiliana vizuri na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Kwa ufuatiliaji endelevu, amesema taasisi na jamii ni vema zikajengewa uwezo na kupewa mafunzo ya matumizi bora na utunzaji wa rasilimali za maji yanayotoka chini ya ardhi. Alisema ufuatiliaji huu utakuwa na mafanikio endapo zana za ufuatiliaji wa maji chini ya ardhi zitapatikana kwa bei nafuu ili ziweze kufikiwa na kila mtu.

Amesema kampuni hiyo inatoa huduma ya maabara ya ufuatiliaji wa ubora wa maji kwa bei nafuu na huduma hiyo inasaidia katika ufuatiliaji wa maji ya ardhini.

# Wanafunzi wanufaika maji ya Ziwa Victoria

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi Masengwa wilayani Shinyanga, wameondokana na matumizi ya maji machafu ya kwenye mabwawa, mara baada ya kutekelezewa mradi wa majisafi na salama kutoka Ziwa Victoria.

Wanafunzi walibainisha hayo juzi wakati wakizungumza na Nipashe ilipotembelea shuleni hapo.

Miongoni mwa wanafunzi hao akiwamo Kulwa Dotto walisema awali kabla ya kutekelezewa mradi huo wa majisafi na salama mwaka juzi, walikuwa wakitumia maji machafu ya kwenye mabwawa na kuhatarisha afya zao ikiwamo kuugua matumbo.

Pia alisema wanafunzi wa kike walikuwa wakipata tabu katika matumizi ya majisafi na salama hasa kujisafisha na hedhi, lakini baada ya kupata maji hayo shida hiyo haipo tena na wamekuwa wasafi muda wote.

"Kabla ya kupata majisafi na salama hapa shule tulikuwa tunafuata maji kwenye malambo (bwawa) ambayo siyo salama na wanafunzi tulikuwa tukiugua tumbo sababu tukizidiwa na kiu tunayanywa,"alisema Kulwa.

Mwalimu Twaha Swalehe akizungumza kwa niaba ya Mwalimu Mkuu msaidizi wa shule hiyo, alikiri ukosefu wa majisafi na salama shuleni hapo ilikuwa ni tatizo, na kwamba wanafunzi walikuwa wakiomba ruhusa za mara kwa mara wakisumbuliwa na matumbo.

Alisema lakini sasa hivi baada ya kupata majisafi na salama, hakuna tena wanafunzi kuomba ruhusu kuumwa matumbo, na wamejenga chumba maalumu cha wanafunzi kujisitiri na hedhi, na watakuwa wakitumia majisafi na salama na kuwa salama kiafya.



# Ahukumiwa kumlipa mkewe milioni 15/-

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Arusha imemhukumu kifungo cha miaka minne jela na kumlipa fidia ya Sh. milioni 15 mke wake, Veronica Kidemi (30) baada ya kukutwa na hatia ya kujaribu kuua.

Hukumu hiyo imetolewa dhidi ya aliyekuwa mfanyakazi wa Shirika la Umeme (TANESCO), Ombeni Alfayo ambaye alimkata mke wake na sime kiganja cha mkono wake wa kulia kutokana na wivu wa mapenzi.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Tanzania Kanda ya Arusha, Joachim Tiganga aliyefafanua kuwa mahakama imeamua kupunguza adhabu ya hukumu hiyo baada ya mshtakiwa Alfayo kukiri mahakamani kutenda kosa hilo na hana rekodi nyingine ya uhalifu.

Akinukuu hukumu mbalimbali zilizotolewa na mahakama nyingine tofauti, Jaji Tiganga alisema kuwa kwa kosa alilofanya Alfayo, alistahiki kuhukumiwa kifungo cha maisha jela lakini kwa kuwa mshtakiwa ambaye alikuwa ni mume wa Veronica (30) hana rekodi za kushtakiwa na ni kosa lake la kwanza, pia ana watoto wawili kwa mke wake, mahakama imeona ni kheri kumpunguzia adhabu hiyo.

Jaji Tiganga alisema kwa kuwa shtaka lake ni la kujaribu kuua chini ya kifungu namba 211 cha sheria, mahakama imezingatia kosa alilolofanya pamoja na alichokisema mahakamani wakati wa kujitetea.

"Kosa ulilofanya lilistahiki ufungwe maisha na kwa kuwa hujasumbua mahakama, ulikiri kosa ninakuhukumu miaka minne jela na fidia ya Sh. milioni 15 umpe mkeo ili kupunguza machungu aliyopata na utetezi wako uliomba usipewe adhabu kubwa sababu una watoto.

"Sasa kwa sababu hujasumbua mahakama, mahakama imekutia hatiani kwa kutumikia kifungo cha miaka minne jela," alisema.

Akipitia ushahidi kabla ya kutoa hukumu hiyo, Jaji Tiganga alisema mshtakiwa Alfayo aliomba mahakama impunguzie adhabu ya hukumu yake kwa sababu ana watoto wawili aliowapata na mke wake, hivyo mahakama imemtia hatiani kwa kumfunga kifungo cha miaka minne jela na kumlipa fidia mke wake ya Sh. milioni 15 kutokana na maumivu aliyomsababishia.

Hukumu hiyo ilitolewa jana mahakamani huko baada ya kuripotiwa kwa tukio hilo Septemba 25, 2020 mshtakiwa alipotenda kosa hilo.

Awali kabla ya kutolewa hukumu hiyo, Mawakili wa Werikali Grace Medikenya na Charles Kagirwa waliiomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali kwa mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwa wanaume katili wanaopiga wake zao.

Hata hivyo, Wakili wa Mshtakiwa aliomba mahakama kumpunguzia adhabu kuwa kuwa hilo ni kosa lake la kwanza na ana watoto wawili ambao alizaa na mke wake, Veronica.

Ombeni alikuwa mfanyakazi wa TANESCO jijini Dar es Salaam na alirejea jijini Arusha na kumpiga mke wake, Veronica Septemba 25 mwaka 2020, akilazwa Hospitali ya Selian wilayani Arumeru mkoani Arusha.

Veronica ambaye ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Kiranyi na Mkazi wa Kijiji cha Siwandeti, alipigwa na mume wake kutokana na wivu wa mapenzi.

Katika kuwasilisha ushahidi wake, mwalimu huyo alidai mumewe alikuwa na tabia ya kumtukana matusi mazito mara kwa mara na kumpiga kwa vitu vyenye ncha kali na wakati mwingine alimnyang'anya watoto wao wawili.

Alidai kuwa siku ya tukio alitoka kazini saa 11:00 jioni kwenda eneo la Mianzini jijini Arusha kutoa fedha za kununua mahitaji mbalimbali ya kifamilia na baada ya hapo alikwenda nyumbani kwake kupika chakula.

"Nilipoingia nyumbani kwangu, mume wangu nilimkuta ndani, aliponiona akaanza kunitukana huku akinikata mapanga na katika harakati za kukwepa nilishtuka mkono wangu wa kulia, umekatwa ukiwa umening'inia," alidai mama huyo.



Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, David Lekei (wa pili kulia), akizungumza na Menejimenti ya Kampuni ya African Plantation Kilimanjaro (APK) na wawakilishi wa vyama vya ushirika wa mazao ya kilimo (AMCOS) jana, kabla ya kugawa magunia 300 ya mahindi kwa ajili ya chakula cha mchana katika shule za msingi 42. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Kampuni yajitosa chakula shuleni

**Na Godfrey Mushi,** HAI

KAMPUNI ya kilimo ya African Plantation Kilimanjaro (APK) imewatua wazazi mzigo wa kuchangia gharama za chakula shuleni kwa miezi mitatu wilaya za Hai na Moshi Vijiji mkoani Kilimanjaro.

APK imetoa magunia 300 ya mahindi ya chakula sawa na tani 30 kwa ajili ya shule za msingi 42.

Akizungumza jana katika hafla ya kukabidhi mahindi hayo, Meneja Mkuu wa APK, Donald Temba alisema mahindi hayo yanayozalishwa na kampuni hiyo iliyowekeza katika kilimo cha kahawa, yatawanufaisha wanafunzi 10,367.

Alisema katika eneo la Moshi Vijijini, shule tatu zilizoko katika eneo linalozungukwa na Chama cha Ushirika wa Kilimo na Chakula cha Kirima Boro AMCOS, zitanufaika, zikiwa na wanafunzi 1,259 waliopatiwa magunia 36 za mahindi ya chakula, Chama cha Ushirika cha Ukiko, wao shule saba zenye wanafunzi 1,619, wamepatiwa magunia 47 ya mahindi na Chama cha Ushirika cha Manushi-Narumu, shule tatu zenye wanafunzi 1,068 zimenufaika kwa kupewa magunia 31.

Alisema Chama cha Ushirika wa Kilimo na Chakula cha Lyamungo AMCOS kinachozungukwa na shule saba za msingi zenye wanafunzi 1,237, kimepata magunia 36 ya mahindi, Chama cha Ushirika cha Manushi-Narumu AMCOS chenye shule sita zenye wanafunzi 1,981 kimepata magunia 57.

Chama cha Ushirika cha Kyumasha kinachozungukwa na shule nane za msingi, zenye wanafunzi 1,649, kimepata magunia 48 na Chama cha Ushirika cha Fonrwa AMCOS kilichoko Kata ya Machame Magharibi, kimenufaika na mpango huo baada ya kupokea msaada wa magunia 45.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, David Lekei alisema mahindi hayo yanatosheleza kutumika katika shule 42 za msingi kwa muda wa miezi mitatu.

# Serikali kuongeza kasi ya mawasiliano

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi amesema serikali imejipanga kuongeza wigo wa mawasiliano ya kasi kutoka asilimia 45 iliyopo sasa hadi kufikia asilimia 80 ifikapo mwaka 2025.

Ndejembi aliyasema hayo jana wakati akifungua kikao kazi cha tatu cha Serikali Mtandao (e-GA) unaoendelea jijini hapa.

Alisema kuwa kupitia TEHAMA, dunia hivi sasa imekuwa kijiji, hivyo pamoja na kupanua wigo huo, pia imejipanga kuongeza kasi ya kufikisha miundombinu ya mkongo wa taifa kwenye maeneo mengi nchini hususan katika ngazi za wilaya.

"Katika dunia ya kiuchumi tuliopo sasa, TEHAMA ni nyenzo wezeshi na kwa umuhimu huu serikali imewekeza na kuweka kipaumbele kwenye matumizi ya TEHAMA kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa kujenga miundombinu ya mfumo tumizi na kisekta ili kusaidia kuboresha ufanisi na uendeshaji wa shughuli zake," alisema Ndejembi.

Aliitaka mamlaka hiyo kuendelea kufanya utafiti ili kuleta ubunifu wa mifumo ya TEHAMA itayoliwezesha taifa kufanikisha kuimarisha sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji pamoja na kulipekeka taifa mbele kimaendeleo.


Alisema Rais Samia Hassan Suluhu wakati akihutubia Bunge kwa mara ya kwanza, alieleza bayana kuwa serikali yake itatoa kipaumbele kwenye matumizi ya TEHAMA hususan katika masuala ya utafiti na ubunifu ili kuimarisha usalama wa mtandao wa mawasiliano, kuongeza watumiaji wengi kutoka asilimia 43 na kuweza kufikia asilimia 80 ifikapo 2025.

"Ili kutimiza azma hiyo ya Rais, nitoe wito kwenu ninyi washiriki kutoa maoni yenu, ushauri na mapendekezo katika kikao hiki yatayowezesha serikali kutekeleza jitihada za serikali mtandao wenye tija, ufanisi na zinazoboresha utoaji wa huduma bora kwa umma pamoja na kutoa mchango katika maendeleo ya taifa letu," aliagiza.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Benedict Ndomba alisema mamlaka hiyo inaendelea kusimamia na kuhimiza uzingatiaji wa sera, sheria, kanuni, viwango na miongozo ya serikali mtandao kwa taasisi za umma ambapo wameendea kutoa miongozo mbalimbali ya kiufundi ili kuhakikisha kuwa matumizi ya TEHAMA katika taasisi za umma yanakuwa na tija ikiwamo kusaidia katika utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa umma.

"Katika kipindi hiki tumetekeleza jukumu la kufanya ukaguzi wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu matumizi sahihi na salama ya TEHAMA serikalini ili kuhakikisha usalama wa mifumo na katika kutekeleza jukumu hili tumeweza kubaini matishio ya kiusalama mtandaoni yapatayo 459 sambamba na kufanya ukaguzi na tathimini za usalama wa mifumo katika taasisi za umma," alisema Mhandisi Ndomba.

Alisema mpaka sasa mamlaka imetengeneza zaidi ya tovuti 300, kuunganisha taasisi za serikali 394 kutoka sekta mbalimbali katika mtandao wa serikali ambao ni salama na gharama nafuu, pia wametoa masafa ya intanet kwa taasisi za umma 554.





# Wadau waonya wazazi watoto kulea wenzao

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WADAU wa maendeleo mkoani Shinyanga wamekosoa vikali tabia ya baadhi ya wazazi na walezi hususani maeneo ya vijijini kuwaachia watoto wao wakubwa kuwalea wadogo zao huku wao wakienda shambani, wakionya kuwa kunawafanya watoto wakose muda wa kujisomea wanapokuwa nyumbani.

Mkurugenzi wa Shirika la WEADO, Eliasenya Nnko alitoa angalizo hilo juzi alipotoa elimu ya ukatili kwa wazazi Kata ya Lyabukande wilayani Shinyanga pamoja na kuunda mabaraza ya watoto ili wapaze sauti kuhusu vitendo vya ukatili.

Alisema wazazi na walezi hususani jamii ya wakulima, wamekuwa na tabia ya kuwaachia watoto wao wakubwa kulea wadogo zao na wao kwenda shambani kulima na kusababisha watoto hao ambao ni wanafunzi kukosa muda wa kujisomea.

"Watoto kuachiwa kulea wadogo zao ni ukatili mkubwa kwa kuwa wananyimwa haki yao ya kujisomea wakiwa nyumbani na kugeuka kuwa walezi," alisema Nnko.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Lyabukande wilayani Shinyanga, Shadrack Malando alisema suala la watoto ambao ni wanafunzi kuachiwa kulea wadogo zao huwa linatokea katika kipindi cha kilimo na hiyo inasababishwa na jamii kuwa na mwamko mdogo wa elimu.

Alisema hatua ambayo wameichukua serikalini ni kushirikiana na wadau wa maendeleo kutoa elimu kwa wananchi kuacha tabia ya kuwafanyia watoto vitendo vya ukatili wa kijinsia na kujua umuhimu wa elimu.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Lyabukande, Jeremiah Mashaka alisema tabia ya wazazi kushindwa kuwapatia watoto wao muda wa kujisomea wanapokuwa nyumbani ni moja ya sababu ambazo zimekuwa zinachangia matokeo mabaya kwa wanafunzi.

# Kikongwe wa miaka 80 adaiwa kunajisi mjukuu

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

LUHENDE Tugwa (80), mkazi wa Kijiji cha Ihapa, Kata ya Oldshinyanga, Manispaa ya Shinyanga, anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kumnajisi mjukuu wake anayesoma darasa la kwanza mwenye umri wa miaka minane (jina tunalihifadhi) na kumsababishia maumivu makali sehemu za siri.

Tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa nne asubuhi wakati bibi yake akiwa shambani na mtoto huyo aliporejea nyumbani kutoka shuleni na kumkuta babu yake ambaye alimnajisi na kumharibu sehemu za siri.

Akisimuliza tukio hilo, bibi wa mtoto huyo, Mariam Kishiwa alisema aliporejea nyumbani kutoka shambani, alimkuta mjukuu wake akiwa katika hali mbaya, akamuuliza kama anaumwa na kupatiwa mrejesho kuwa sehemu za siri kuna tatizo na alipomwangalia akabaini alikuwa anatokwa na damu.

Alisema ilibidi atoe taarifa kwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Oldshinyanga ili kujua kilichomkuta mjukuu wake kwa kuwa wakati anaondoka kwenda shambani, mjukuu wake huyo alikuwa shuleni.

"Tulipomwangalia na mwalimu, tukagundua amebakwa, ndipo tukampeleka hospitalini kufanyiwa vipimo ambavyo pia vilionyesha alibakwa," alidai bibi huyo.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Judithi Julius alisema mtoto huyo aliondoka shuleni akiwa salama, hivyo ubakaji huo ulifanyika nyumbani kwao kwa kuwa hata walipomhoji mwanafunzi mwenyewe, alidai kufanyiwa ukatili huo nyumbani kwao.

Diwani wa Viti Maalum Kata ya Oldshinyanga, Pica Chogelo alilaani tukio hilo na kuomba vyombo vya dola viwashughulikie watu ambao wamekuwa wakiwafanyia watoto vitendo vya ukatili ambavyo pia vinawaathiri kisaikolojia.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kubainisha kuwa wanamshikilia babu wa mtoto huyo na uchunguzi utakapokamilika atafikishwa mahakamani ili kuchukuliwa hatua zaidi za kisheria.




Madiwani wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, wakiwa kwenye kikao cha kawaida cha robo tatu ya mwaka, wakijadili ajenda mbalimbali zikiwamo za miundombinu ya barabara, elimu, umeme, maji na afya kwa ajili ya mustakabali wa maendeleo ya wananchi wa manispaa hiyo, jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# EWURA watoa vifaa tiba Hospitali ya Nyamagana

**Na Richard Makore,**
MWANZA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imetoa msaada wa vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni tano kwa Hospitali ya Wilaya ya Nyamagana (Butimba) kupitia fungu la uwajibika kwa jamii (CSR).

Akizungumza katika kikao cha tano cha Baraza la Kwanza la Wafanyakazi wa EWURA kilichofanyika jijini Mwanza juzi, mwenyekiti wa kikao hicho, Poline Msuya alisema wamekuwa na utaratibu wa kuipatia jamii vitu vya msingi wanapokuwa na nafasi kifedha kufanya hivyo. Msuya alisema kama sehemu ya kutambua jitihada za serikali, hususani katika sekta ya afya, EWURA imeona ni vyema kutoa msaada wa vifaa tiba kwa Hospitali ya Wilaya ya Nyamagana.

Alifafanua kuwa fedha hizo zitagharimia mashine sita za kupimia shinikizo la damu (BP Machine digital) zenye thamani ya Sh. 426,000, viti viwili vya magurudumu kwa ajili ya kusaidia wagonjwa vyenye thamani ya Sh. 709,000, vitanda vinne vya uchunguzi vyenye thamani ya Sh. 1,917,200 pamoja na vifaa 10 vya kujifungulia vyenye thamani ya Sh. milioni 2.1.

Alisema ni wajibu wao kuhakikisha upatikanaji wa huduma zinazodhibitiwa na EWURA, ambazo ni huduma za nishati na maji zinapatikana kwa wakati na kwa gharama nafuu. Akizungumza baada ya kupokea msaada huo, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Dk. Pima Sebastian aliishukuru EWURA kwa kuunga mkono jitihada za serikali katika sekta ya afya kwenye wilaya hiyo.

Dk. Pima alisema hospitali hiyo inatoa huduma kwa wawawake 650 hadi 750 kwa mwezi na inapokea wagonjwa wa nje 8,000 mpaka 12,000 na wajawazito 3,500 hadi 5,000.

Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, alipongeza EWURA kwa kuiunga mkono serikali kwa vitendo.

Alisema anaifahamu EWURA kwa muda mrefu na imekuwa inafanya kazi kwa weledi kuhakikisha jamii inanufaika.

"Mmekuwa mkidhibiti bei ya maji na mafuta, ninawawafahamu kabisa wala sina shaka na ninyi, mnafanya kazi nzuri sana kwa jamii," alisema


Aliwataka wafanyakazi wa EWURA kufanya kazi kwa weledi kwa kuwa taifa linawategemea ili kuwapatia unafuu kupitia huduma wanazosimamia za nishati na maji.



Ukurasa 12

**PAJUE MAKARAI MWANZA – FUNDI HALALI NJAA!**

Kiwanda kidogo kilichosheheni mafundi mchundo, siri ajira binafsi, darasa la mamia mafundi wapya




Ukurasa 13

Usuluhishi wa migogoro uwe wa lazima



Ukurasa 14

**Ijue PPRA inavyosimamia zabuni ya ununuzi umma, hadi utekezaji**

BUFE
IJUMAA FEBRUARI 10, 2023
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

UCHUMI

# Rais alipoelekeza urafiki na walipa kodi, ikamjibu na pato rafiki kitaifa

- Hakuna biashara kufungiwa, azuia riba kodi ardhi...

**Na Mwandishi Wetu**

MUASISI wa taifa Mwalimu Julius Nyerere, katika hoja zake amekuwa akisisitiza umuhimu wa serikiali kuwa na ufanisi na si rushwa kuamua zaidi katika kukusanya kodi ikipiga hatua maradufu ya uwezo wa kuhudumia umma

Kuna mambo kadhaa yamechukua nafasi tangu Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kuingia madarakani miaka miwili sasa. Inapoangaliwa undani wake, anajikita kuipa biashara uhai, kutanua wigo mpana wa uzalishaji viwandani na nje ya viwanda, kama vile shambani.

Eneo lingine linalofungua mtazamo ni katika kufungua milango ya kibiashara kimataifa. Katika hilo, Dk. Samia amekuwa akichukua juhudi binafsi kuhamasisha mwenyewe kuinua uhamasishaji, ushuhuda wake ukibebwa na ziara kimataifa.

Kwa sura moja, wapo waliompinga dhidi ya hatua hizo za kusafiri kwamba inaibebesha taifa mzigo mkubwa wa gharama ya matumizi ya umma, hatua ikamlazimu wakati fulani kuitolea ufafanuzi manufaa yake katika mustakabali huo wa gharama kitaifa.

Mara zote kwa asilimia kubwa, serikali inabaki kwenye wajibu wake wa asili kuwa mhamasishaji, mratibu na msimamizi mkuu kisheria katika uendeshaji shughuli za kiuchumi kitaifa, huku wawekezaji binafsi katika ngazi mbalimbali kuanzia juu hadi chini wakulima na wajasiriamali ndio washiriki wakuu.

Hata hivyo, kuna baadhi ya miradi ya kiuchumi na maeneo ya kuhudumia taifa, serikali huwa mshiriki wa moja kwa moja, mathalani Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) na Shirika la Reli (TRC) zinamilikiwa, pia kuendeshwa na serikali.




Watumishi wa Mamlaka ya Kodi Tanzania, wakihamasisha ulipaji kodi kwa hiari, ,mkoani Simiyu. **PICHA: MTANDAO**

Vivyo hivyo, Rais Dk. Samia kuna wakati ukachukua hatua ya kuhamasisha utalii, akashiriki katika kuandaa sinema ya Royal Tour, iliyomlazimu kusafiri hadi kufika ughaibuni katika nchi mbalimbali kurekodi, sasa mafanikio yake yanashuhudiwa kwa kumiminika watalii nchini.

Hayo yote kiuchumi yana mantiki kadhaa: kuamsha shughuli za kiuchumi na biashara zikapata uhai; kupanua wigo wa ajira za ndani; mzunguko wa fedha na pato la moja kwa moja la serikali, vilevile kutunisha chanzo kikuu cha pato la serikali ambayo ni kodi, kama alivyosisitiza Mwalimu Nyerere na hata watangulizi wengi duniani.

**MAKUSANYO YANAENDESHWAJE?**

Katika mwenendo huo wa maboresho kuandaa mazingira wezeshi kiuchumi na kibiashara nchini, Rais Dk. Samia, akaelekeza kuwapo mabadiliko makubwa katika mfumo wa ukusanyaji kodi kutoka vyanzo na sekta binafsi, ikiwamo kwa wafanyabiashara.

Moja ya mambo ambayo rais akapiga marufuku, ya kufunga biashara na kuzuia akaunti za wafanyabiashara uliokuwa umetawala na badala yake kukaa meza moja kutafutia majibu namna kodi zinazodaiwa zitawasilishwa.

Katika hilo akalitolea ufafanuzi kwamba, biashara na mifumo husika ya kiuchumi inatakiwa kuachiwa mazingira ya kujiendesha, ili kupata uwezo wa kulipa kodi na daima si kufungiwa.

Ni hali iliyojionyesha mara moja kutoka kwa walipa kodi, huku TRA ikianzisha kampeni rafiki katika ukusanyaji kodi, aina ya hatua inayoendelea hadi sasa.

Mnamo, Januari mwaka huu, TRA ikatangaza mafanikio makubwa kupitia mfumo huo, ikikusanya kupitia kodi jumla ya shilingi trilioni 12.4 katika nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/2023, ni sawa na asilimia 99 ya lengo la makusanyo ya Sh12.48 trilioni.

Pia, inaelezwa makusanyo ya mwezi Desemba mwaka jana, ambayo ndio maelekezo ya Rais yamekuwa yakiendelea kufanyiwa kazi, yamevunja rekodi tangu kuanzishwa kwa mamlaka hiyo mwaka 1996.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kamishna Mkuu wa TRA, Alphayo Kidata, makusanyo hayo ni ongezeko la shilingi trilioni 1.35, ikilinganishwa na shilingi trilioni 11.11 iliyokusanywa kwa kipindi kama hicho mwaka wa fedha uliopita. Ni taarifa inayotaja kuwapo ongezeko la mapato yakikua kwa asilimia 12.2.

Kwa mujibu wa TRA ni kwamba, katika mwenendo huo wa ulipaji kodi kwa hiari kama ilivyoelekezwa na Rais, pia uhusiano baina ya mamlaka na walipakodi, umeendelea kuimarika kwa kiwango cha kuridhisha.

Katika hilo, TRA kupitia taarifa yake inaendelea kufanyia kazi malekezo na miongozo ya Rais kuhusu namna bora ya kukusanya mapato pasipo kufanyika

INAENDELEA UK.14

BIASHARA

IJUE MAKARAI MWANZA ILIKO 'FUNDI HALALI NJAA!'

# Kiwanda kidogo kilichosheheni mafundi mchundo, siri ajira binafsi, darasa la mamia mafundi wapya

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

BIASHARA, uchumi na fedha,ni mambo muhimu matatu yanayoenda sambamba katika maendeleo ya watu na nchi kwa ujumla kote duniani.

Bila kuwapo mambo hayo maendeleo hayawezi kusonga mbele katika mtu mmoja mmoja au jamii nzima, kama anavyobainisha kiongozi wa mafundi katika kiwanda kidogo cha kutengeneza malighafi mbalimbali za biashara.

Maulid Madata, ni Mwenyekiti wa mafundi katika chama cha Pangoni Group katika kiwanda kidogo cha makarai kilichopo Butimba A, jijini Mwanza, eneo maarufu kwa jina la Makarai, ambako kunatengenezwa bidhaa za namna hiyo na kuuzwa rejareja na jumla.

Fundi Madata anajigamba akirejea tamko la wahenga 'fundi hawezi kulala njaa.' Hapo anasema kwamba ,kwa kuzingatia ubunifu, kanuni na maarifa, ndiyo njia pekee inayomfanya fundi stadi wa vyuma vya kuchoma,ujenzi na vitu vingine kuwaingizia kipato cha kila siku.'

Anajitambulisha kitaaluma kuwa fundi wa kutengeneza sahani za mizani ya kuuzia vyakula; mchele, sukari, maharage, viazi mviringo na vinginevyo, akitaja bei yake ya uuzaji ni kati shilingi 5,000 hadi shilingi 7,000 kulingana na ukubwa wake, hivyo anasema kila siku ni kawaida hakosi chochote kinachoingia mfukoni.



Juma Nassoro, fundi masanduku akionyesha bidhaa hiyo kiwandani. **PICHA ZOTE: ANTHONY GERVAS**

**UMAARUFU WAKE**

Eneo kilipo kiwanda hicho kidogo ni maarufu kwa jina la 'Makarai' kutokana na kutengeneza makarai kwa wingi wa bidhaa zingine mbalimbali zilizosheheni pale, watu wengi wakiwamo wafanyabiashara wadogo huenda kununua bidhaa hizo.

Kiwanda cha Makarai kinatengeneza makarai, masanduku ya nguo wanafunzi shuleni, majiko, kabati za kuuza sambusa, makaangio ya samaki, dagaa, vitumbua na chapati, ndoo na vifaa vya kuweka keki huwafikia wateja kwa njia ya rejereja na jumla.

Madata anasema ameianza kazi ya ufundi mwaka 1983 na hadi sasa imemsaidia maisha yake na familia hata amejenga nyumba anayoishi, anasomesha watoto shule. Hivyo, anakiri hakusomea fani hiyo, bali alijifunza mwenyewe na hata akamua kujiajiri.

Hivi sasa akiwa mwenyekiti katika kiwanda cha Makarai, anasema ameamua kuwasaidia vijana na watu wengine wanaopenda kujifunza ufundi, akitoa fursa ya bure kiwandani hapo,ili kuwanusuru hasa vijana na maisha ya uzururaji na wizi.

> **"Makarai wanayotengeneza yanatokana na malighafi za mapipa chakavu yaliyotumika kutengenezea barabara za lami, wao hununua na kuunda bidhaa hizo za makarai, vikaango na majiko.**

Anafafanua ni hatua ya kupanua wigo wa ajira kwa vijana, akiwakaribisha hata wanawake kuingia kwenye fani hiyo kiwandani,ili baada ya kufahamu ufundi itakuwa fursa yao kujiajiri.

Vilevile anasema kuwa itawawezesha kuanzisha viwanda vyao vidogo na kuwafundisha vijana wengine, wakiwamo wanawake ambao si wengi katika fani hiyo akiisifu fani hiyo 'inalipa,' mwenyewe akijivuina kwa hoja 'ufundi hauzeeki.'

Ana angalizo pia, kwamba ufundi ni kazi ngumu inayohitaji kipaji, akili nyingi,maarifa na ubunifu, ili kuendana na soko la bidhaa zinazohitajika wakati huo, akisema wapo wanaoishia kuigusa fani hiyo na kuikimbia, kwa sababu inahitaji uvumilivu katika hatua ya mwanzo.

Fundi Madata anaitaka jamii iache tabia ya kuchagua kazi,kusubiri kuajiriwa na serikali, badala yake wajiajiri hasa vijana, kwani fursa za ajira ni kidogo ikilinganishwa na uhitaji wake, hivyo kujiajiri wenyewe inabaki kuwa njia suluhishi itakayowasaidia kujikwamua kimaisha.

**SOKO LIKOJE?**



Mwenyekiti wa Mafundi katika kiwanda kidogo cha makarai, Pangoni Group, Maulid Madata, akiendelea kuunda sahani za mzani.

Madata anaeleza kuhusu masoko ya kuuzia bidhaa zao wanazotengeneza yapo ndani na yanatosha kulingana na kiwango chao cha ujuzi, ubora wa malighafi wanazotengeneza.

Fundi Madata anafafanua kwamba, kwa sasa siyo rahisi kuuza nchi za nje katika soko la ushindani sababu vifaa wanavyotumia kutengenezea ni duni zikiwamo nyundo.

Anasema kiwanda cha Makarai, kilianzishwa mwaka 1992 na hadi sasa kimeshafundisha zaidi ya vijana 200 ambao sasa ni mafundi 200 kamili, baadhi yao wapo kiwandani, idadi yao ni 60, wakitawanyika katika fani mbalimbali.

Ikiwa ni pamoja na uchomaji vyuma na utengenezaji wa kofia za kuezekea nyumba za bati, huku akinena hakuna kazi isiyokuwa na changamoto bali kinachotakiwa ni uvumilivu tu.

**MAFUNDI WALIONOLEWA**

Ekonia Charles, ni kijana mwenye umri wa miaka 42, mkazi wa Majengo Ibanda, jijini Mwanza, anasimulia kuwa yeye kazi ya ufundi ametimiza miaka 10 na hakuendea kusoma chuoni, amejifunza mwenyewe na akajiajiri, yuko katika Kiwanda cha Makarai, akiwa mtaalamu wa kutengeneza karai.

Charles anasema, kuna karai anazounda ndogo na kubwa, akiziuza moja shilingi 15,000 hadi 35,000 na makubwa yenye ujazo wa lita 20, anatumia nyundo nzito na kwamba ni kazi ngumu, akitaja ni sharti awe amekula na kushiba, kwa sababu anatumia nguvu nyingi kazini.

Pia, anaeleza kuwa kila siku hutengeneza karai ndogo kuanzia 10 hadi 12 na makubwa wastani wa manne, kwamba zinamsaidia kuingiza kipato cha kusomesha watoto shule na anauza kwa siku kati ya karai 10 hadi 15 kulingana na soko, linapodorora anaishia kuuza karai mbili tu.

Anasema, makarai wanayotengeneza yanatokana na malighafi za mapipa chakavu yaliyotumika kutengenezea barabara za lami, wao hununua na kuunda bidhaa hizo za makarai, vikaango na majiko.

Katika fani yake hiyo ana malengo ya kutafuta mtaji wa kufanya biashara mbalimbali, pia anaomba serikali iwape vijana mikopo yenye masharti nafuu, kwa ajili ya mitaji ili waweze kujiajiri na kujikwamua kiuchumi wakiwa bado wana nguvu nyingi.

Juma Nassoro, mkazi wa Mkuyuni jijini hapa, ambaye pia ni fundi wa kutengeneza masanduku ya nguo ya wanafunzi shuleni, anasimulia ujuzi wake aliupata kwa njia ya kujifunza mwenyewe katika viwanda vidogo, katika kijiji cha Goweko mkoani Tabora mwaka 1994. Sasa ni fundi kamili.

Anaisimualia Nipashe kuwa, alianza kujifunza baada ya kumaliza darasa la saba mwaka 1983 na baadaye akafika jijini Mwanza,mwaka 1998, akiendelea na kazi hizo za kiufundi akijiajiri.

Huwa anaunda masanduku, akitamba yapo katika kiwango sawa na viwango vya vinavyoundwa kutoka kwenye Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO), akitumia malighafi mabati yaliyoharibika wakati wa uzalishwaji kiwandani.

Nassoro anasema huwa ananunua mabaki ya mabati hayo kutoka viwanda vya kutengeneza mabati na kutengeneza masanduku ambayo bati moja lenye urefu wa futi 10 huuzwa shilingi 25,000 yeye ana uwezo wa kutengeneza kwa siku masanduku sita na kila moja anauza kwa bei shilingi 20,000.

Anasema, changamoto kwake ni nyenzo wanazotumia katika ufundi kuwa ni duni,akitaja nyundo na vitu vingine na kuna wakati upatikanaji wake unakuwa shida, akitaja baadhi ya malighafi kama mabati viwandani, analazimika kuzitafuta chakavu.

Manufaa anayataja kwamba, kazi ya ufundi imemsaidia kujenga nyumba yenye thamani ya vyumba vinne, ikihudumia familia yake, wanawe wanapata elimu,sasa akiwa na malengo ya kujenga nyumba nyingine ya kuwekeza kitega uchumi kama vile maduka kupitia fani hiyo.


Fikiri Maganga, yumo katika miongoni mwa mafundi hao wa makarai yeye kazi hiyo, naye anaifanya kwa malengo, ili baadaye apate mataji aweze kuwekeza kwenye kilimo cha alizeti, ambacho anaona kwake kina tija kuliko ufundi anaofanya.

"Malengo yangu baadaye ni kufanya kazi ya kilimo cha alizeti, pamoja na kwamba ufundi umenipa faida kujenga nyumba ya tope ya kuishi,kazi hii ngumu inahitaji akili,maarifa,zana tunazotumia zinakuwa duni tunatumia inatakiwa mlo wa kutosha," anasema.

Anahitimisha kwamba, kuna wakati anakabiliwa na changamoto ya kujeruhiwa na mabati wanapotengeneza, hivyo hulazimika kujitibu kwa gharama kubwa. Pia, SIDO imekuwa ikiwapa elimu na semina za ujuzi kuhusu kufanya kazi za ufundi kwa ufanisi zaidi.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Usuluhishi migogoro uwe wa lazima






**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**kulangwasos@gmail.com**

FEBRUARI mosi mwaka huu katika maadhimisho ya Siku ya Sheria nchini, niliwasikia Rais Samia Suluhu Hassan na Jaji Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma, wakisisitiza usuluhishi wa migogoro katika jamii.

Wawili hao walizungumza vema sana kuhusu umuhimu wa hatua hiyo, wakisema kwanza inaokoa muda, pia inaimarisha uhusiano baina ya pande mbili zilizo kwenye mgogoro.

Wakasema, usuluhishi unapotumika kabla ya kufikishana mahakamani, uhusiano baina ya walio kwenye mgogoro hubaki ulivyo, kwani huhifadhiana siri, kuliko inavyokuwa mahakamani kila kitu kuanikwa.

Katika kuliimarisha hilo, Rais akaunda Tume ya Haki Jinai itakayofuatilia taasisi mbalimbali za kutenda haki kuona zinavyotenda, pamoja na changamoto zilizomo, ili zitatuliwe ili taasisi hizo zitende haki itakiwavyo.

Hata hivyo, usuluhishi hufanyika katika migogoro ya madai na si ya jinai, hivyo ni vizuri ikaitwa haki madai badala ya haki jinai, katika suala zima la utekelezaji wa usuluhishi katika migogoro ya kijamii.

Mara nyingi usuluhishi umekuwa ukifanyika katika masuala ya madai, kwani jinai mara zote hutatuliwa mahakamani ambako upelelezi hufanyika na ushahidi kutolewa na hatimaye hukumu.

Uzuri mwingine wa usuluhishi kwa mujibu wa viongozi hao wa kitaifa ni kwamba hapatikani mshindi ambaye husababisha mwingine kushindwa na hivyo kuibua chuki baina yao. Kwenye usuluhishi hufikiwa makubaliano na maisha kuendelea.

Watu wengi hujikuta zaidi katika usuluhishi ni katika ajira ambako kuna mwajiriwa na mwajiri na mara nyingi haya hujitokeza pale ajira inapokoma, kwa sababu yeyote, lakini yenye mwelekeo wa uonevu.

Waajiriwa wanaokuwa wameachishwa kazi na kuhisi kuonewa, ndio hukimbilia kwenye tume za usuluhishi (CMAs), ambako kwanza wasimamizi huomba pande mbili za mgogoro kusuluhisha na kwa mazungumzo nje ya mahakama.

Inaposhindikana, ndipo sasa shauri huingia mahakamani na kesi kuanza kama kesi zingine, ambako ushahidi na vielelezo hutakiwa, ili kuthibitisha madai dhidi ya mdaiwa.

Lakini, mara nyingi waajiri ambao ndio huonekana kushika mpini, hukataa usuluhishi na kuamua kusonga mbele kwa shauri kusikilizwa, kwa imani kwamba wanaweza kushindana kuwaacha wadai bila kitu.

Hilo hutokana na waajiri wengi wenye misuli kiuchumi, kuamini kwamba wanaweza kutumia fedha zao kufanya lolote na kushinda, hasa shauri linapokuwa mbele ya wasimamizi wenye uchu wa fedha na hivyo kushindwa kutenda haki.

Kama walivyotanabaisha viongozi wetu hao wawili wa kitaifa endapo usuluhishi utatumika muda utapungua, lakini gharama zitapungua ambazo ni za nauli, chakula, malazi na hata kumlipa mwakilishi (wakili).

Hata hivyo, mawakili wengi hawapendelei usuluhishi, kwa sababu wanajua shauri likimalizika mapema, nao hukosa kipato kwani wapo wanaolipwa kila wakionekana kwenye shauri, hivyo kumalizika mapema ni kukata mrija wa kipato.

Tamaa hii ndiyo imekuwa ikisababisha mashauri kulundikana katika tume hizo na mahakamani, lakini kuchelewesha haki ambako ni sawa na kunyima haki kwa walalamikaji au wadai, katika kesi au shauri husika.

Kama ilivyopendekezwa na baadhi ya wadau, Idara ya Mahakama nchini isimamie hili na kutunga sheria inayolazimisha usuluhishi wa mashauri, badala ya kukimbilia mahakamani, ili kuondoa changamoto hiyo ambayo si tu inaligharimu taifa pekee, ni mateso kwa wananchi.

Ukitaka kuona jinsi Watanzania wanavyoteseka hususan waliokuwa waajiriwa, nenda kwenye tume za usuluhishi na Mahakama ya Kazi, ndipo utaona jinsi watu wanavyohangaikia haki zao, pale wanapokuwa wameondoshwa kazini isivyo halali.

Kwa kuwa mashauri haya ya madai hayahitaji upelelezi kama ilivyo kwa mashauri ya jinai, ni vema usuluhishi ukawa wa lazima, ili kuondokana na kupoteza muda na kama wadaiwa watakuwa wanafanya jeuri kwa kutanguliza misuli ya kiuchumi, basi wanaposhindwa kesi walipe na riba.

Hiyo itakuwa sawa, kwa sababu mara nyingi waajiriwa hudai haki zao ambazo ni mishahara na haki zingine za kifedha, hivyo itokeapo mwajiri akabainika anafanya jeuri hiyo, basi ikionekana ni haki ya wadai wa kulipwa, ukokotoaji wa riba ufanyike ili ilipwe. Alamsiki!

UCHUMI

# Ijue PPRA inavyosimamia zabuni ya ununuzi umma, hadi utekelezaji

**Na Mwandishi Wetu**



Kikao kinachohusu ufungaji wa zabuni ya umeme, kwenye mradi wa Stiegler's Gorge, kilipoendelea Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

KUNA usemi 'mipango siyo matumizi'. Hoja hapo ni vihatarishi vinavyojitokeza katika mpango wa mtu aliyojiwekea, hata ukasabaisha mambo yake ama yasitimie au kuchelewa

Vihatarishi katika michakato ya ununuzi wa umma, ni sehemu ya vikwazo vikubwa katika kufikia azma ya kupata huduma bora katika ununuzi.

Kwa mujibu wa Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA), vihatarishi vinavyojitokeza katika mchakato huo, husababisha malengo ya kitaasisi ama kuharibika au kuchelewa.

Hatua ya mchakato mzima wa ununuzi wa umma hujumuisha wasilisho la kuomba zabuni kwa mhitaji nwenye sifa.

Kuna miongozo mbalimbali ya kisheria na taratibu zimewekwa kwa mujibu wa wadau husika na taaluma hiyo, wakiwamo Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA) na bodi inayohusika na ugavi, pia ununuzi.

Kwa mhitaji huwa kuna utaratibu wa kumdai dhamana za zabuni na utekelezaji wa mikataba yake, taasisi ya ununuzi huweka utaratibu kuwasilisha dai la dhamana za kutekeleza mikataba inayohusu ununuzi na mauzo.

Dhamana nayo kazi yake kubwa ni kutoa hakikisho kutoka kwa mpokea kandarasi anayepatiwa dhamana ya kuwa muuzaji.

Mkurugenzi wa Kujenga Uwezo na Huduma za Ushauri Kutoka Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma(PPRA) Mhandisi Amini Mcharo, anasema dhamana inatumiwa ili kudhibiti hatari ya mzabuni kutofikia malengo.

"Taasisi mnunuzi hudai dhamana kutoka kwa wazabuni ili kujihakikishia wazabuni hawatajitoa katika michakato ya zabuni, kabla ya wakati unaoruhusiwa, watakubali marekebisho ya bei zao, watakubali tuzo za zabuni na kutekeleza mikataba ya ununuzi kwa uaminifu" anaeleza Mhandisi Mcharo.

Anafafanua kuwa dhamana hudaiwa kutoka kwa wazabuni kwenye mchakato wa zabuni na usimamizi wa mkataba; pia zinadaiwa wakati wa usimamizi wa mkataba, ikiitwa 'dhamana za utekelezaji mkataba.'

**KWANINI NI DHAMANA?**

Mhandisi Mcharo anasema inasaidia kuhakikisha mwombaji hataondoa zabuni yake kabla ya zabuni kutolewa kwa mzabuni.

Anafafanua kuwa mzabuni, pia anawajibika kukubali marekebisho ya hesabu za bei kutoka kwa taasisi mnunuzi. Pia, taasisi hiyo itakubali tuzo ya zabuni kama itatolewa iwapo ndiye mzabuni mshindi.

Mcharo anaeleza kuwa dhamana ya utekelezaji mkataba, inalenga kuhakikisha mzabuni mshindi atatekeleza wajibu wake wa kusambaza bidhaa, kutoa huduma au kufanya kazi iliyoanishwa kwenye mkataba wa ununuzi.

"Iwapo mzabuni hatotekeleza mambo ambayo alitoa hakikisho la kuyafanya kwa mujibu wa dhamana aliyoitoa, basi huchukuliwa hatua, ikiwamo kufungiwa kushiriki michakato ya zabuni ya taasisi zote nchini au kutaifishwa kwa dhamana iliyowasilishwa," anasema Mcharo.

**AINA YA DHAMANA**

Mtaalamu wa ununuzi wa PPRA, Frank Yesaya, anaeleza dhamana zinazoruhusiwa kisheria, zimegawanyika katika makundi makubwa mawili; mfumo wa kifedha, pia kwa tamko.

Yesaya, anasema, dhamana za kifedha zinazotolewa na benki na mashirika ya bima; wakati za mfumo wa tamko zinahusisha mzabuni kujaza tamko sanifu lililopo kwenye nyaraka za zabuni, kutoa hakikisho kwa taasisi mnunuzi.

"Ni muhimu taasisi mnunuzi kuthibitisha uhalali wa dhamana za mfumo wa kifedha zinazowasilishwa na wazabuni kutoka benki au mashirika ya bima yanayotoa dhamana husika" anasema Yesaya.

**PENYE UKIUKWAJI**

Yesaya, anasema iwapo mzabuni ataenda kinyume na dhamana ya kifedha, taasisi mnunuzi ina haki ya kuitaifisha dhamana husika na kueleza endapo mzabuni yuko kinyume na dhamana.

Pia, inatajwa penye mfumo wa tamko, taasisi mnunuzi ina haki ya kuomba mzabuni afungiwe na PPRA asishiriki michakato kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka miwili.

"Adhabu zinazotolewa kwa kukiuka masharti ya dhamana zimelenga kuhakikisha wazabuni wanakuwa makini katika utekelezaji wa zabuni zao."

Anasema taasisi mnunuzi inaruhusiwa kuomba dhamana za mfumo wa kifedha, iwapo thamani ya zabuni au mikataba ya ununuzi imefikia kiwango ambacho kinaruhusiwa kuomba dhamana za kifedha.

"PPRA imetoa mwongozo wa dhamana unaotoa maelekezo kwa taasisi nunuzi kuhusu dhamana za zabuni na utekelezaji wa mikataba, kupitia mwongozo huo, imetambulishwa aina mpya ya dhamana ya utekelezaji wa mkataba ambayo ipo katika muundo wa tamko.

"Kwa kuanzia dhamana hii, itadaiwa na taasisi mnunuzi wa mikataba ya ununuzi wa bidhaa, huduma na kazi za ujenzi isiyozidi fedha za kitanzania bilioni moja," anasema.

"Wazabuni huingia gharama kupata dhamana za zabuni zilizo katika mfumo wa fedha, hivyo ni muhimu taasisi mnunuzi kuomba hizo kwa zabuni ambazo zimefikia viwango vinavyoruhusiwa.

Taasisi wanapoahirisha michakato ya ununuzi, huwaingiza wazabuni katika hasara ya kuendelea kukatwa marejesho ya dhamana za kifedha, wakati michakato husika ilishafutwa.

## Rais alipoelekeza urafiki na walipa kodi, ikamjibu na pato rafiki kitaifa

**INATOKA UK.11**

matumizi ya nguvu na kuendelea kujenga mazingira wezeshi ya uwekezaji na kufanyika biashara nchini.

"Serikali imeendelea kuisaidia Mamlaka katika ujenzi na matumizi ya mifumo inayochangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa ufanisi katika utendaji kazi wetu," inaeleza mamlaka hiyo, inayoahidi kuboresha huduma kwa walipakodi kwa kuzingatia uadilifu, weledi na uwajibikaji ili kujenga taswira ya kuaminika kijamii

**SAFARI YA MAFANIKIO**

Mnamo katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba katika mwaka wa fedha, Rais Dk. Samia akiwa hajakamilisha mwaka mmoja katika nafasi ya urais, kukashuhudiwa hatua kubwa ya makusanyo kodi kwa asilimia 98 ya lengo husika, kiasi cha shilingi trilioni 11.11, dhidi ya Sh. trilioni 11.3 zilizolengwa.

Kwa mujibu wa taarifa hizo, katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2020/21 zilikusanywa shilingi trilioni 9.24.

Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na wananchi wa Nyakanazi mkoani Kagera wakati akielekea Mkoani Kigoma leo Jumapili Oktoba 16, 2022.

**ATOA ELIMU**

Rais Dk. Samia naye hakuwa nyuma katika mizunguko yake kuhamasisha wajibu wa kodi kwa hiari, daima huwaachia umma salamu za wajibu wao katika kulipa kodi kwa hiari, kwani ndio chanzo cha fedha za miradi ya maendeleo kitaifa.

Vilevile akatumia nafasi hiyo, kuwahamasisha viongozi mbalimbali wa serikali, wakiwamo mikoani kuendelea kuuhamasisha umma kuwajibika na ulipaji kodi.

Akiwa ziarani wilayani Biharamulo mkoani Kagera Oktoba mwaka jana, Rais Dk. Samia akawakumbusha wakazi kuwa fedha zinazotangazwa na viongozi kutolewa kwa ajili ya miradi mbalimbali kitaifa, zinatokana na kodi za wananchi.

Rais Dk. Samia ameyasema hayo katika eneo la Nyakanazi wilayani Biharamulo Mkoa wa Kagera akiwa njiani kuelekea mkoani Kigoma, alipokuwa akijibu maswali ya Mbunge wa jimbo hilo. Huku akiwaonya wanaokaidi kulipa kodi, Rais Dk. Samia anafafanua: "Mkilima vizuri mkauza mazao tunakusanya, mkichimba madini tunakusanya, ukiwa na duka lako 'kijikodi' kidogo tunakusanya."

**RC ASHIRIKI**

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Yahya Nawanda, baada ya kupokea maelekezo ya rais, viongozi serikalini wakahamasisha ulipaji kodi, Novemba mwaka jana, akawaagiza maofisa TRA mkoani, watoe elimu kwa wafanyabiashara kuhusu ulipaji kodi kwa wakati na hiari.

Akiwa mjini Bariadi, anasema ni lazima maofisa hao wahakikishe wanatengeneza mazingira wezeshi kwa kila mdau alipe kodi.

"Kuweni na lugha nzuri mnapowafuata wateja, wananchi wengi wanahitaji elimu ya mlipa kodi, ili waelewe umuhimu wa kulipa kodi kwa wakati," anasema Nawanda.

**KODI ARDHI**

Kuhusu kodi ya ardhi nako kumekuwa na kiasi kingi ambacho kimekuwa hakijalipwa, Rais Dk. Samia akatumia nafasi yake kusamehe riba kwa wadai ambao wangekuwa hawajalipa hadi kufika Julai mwaka jana, msamaha huo wa bila riba, umedumu hadi Desemba mwaka jana.

"Wale ambao madeni yao yana miaka mitano kurudi nyuma watalipa bila ile tozo ya riba" akatamka Waziri wa Ardhi, Nyumba na Makazi, Dk. Mabula, akiongeza :"Mama Samia ameridhia kupitia Waziri wa Fedha kwa kushirikiana na Waziri wa Ardhi, waweke utaratibu mzuri wa ninyi kuondolewa tozo ile na msamaha ni wa miezi sita tu (hadi Desemba 2022).

"Kama una ndugu mpigie simu mwambie serikali ya awamu ya sita chini ya mama Samia imetoa msamaha kwa wadaiwa sugu ili watoke katika jina baya la wadaiwa sugu kwenda kulipa madeni bila riba."

Wiki hii kupitia uamuzi huo wa Rais Dk. Samia, Serikali imeongeza tena muda wa ulipaji kodi ya pango la ardhi wenye msamaha wa riba hadi kufikia Aprili mwaka huu.



# RC aonya visingizio kwa makandarasi

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma amewataka makandarasi kuacha visingizio visivyo na tija wanapochelewesha miradi wanayotekeleza kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Rosemary Senyamule alitoa onyo hilo jana baada ya kushuhudia utiaji saini wa mikataba ya utekelezaji wa mradi wa maji Nzuguni jijini hapa kati ya makandarasi wanne na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA).

Rosemary aliwataka makandarasi hao kuacha visingizio wanapochelewesha kazi kwa kuwa kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi hiyo, walishafanya ukaguzi wa eneo la kazi.

"Mkandarasi akichelewesha kazi, utasikia 'tulikwamishwa na mvua', hivi wewe wakati unatia saini mkataba wa kufanya kazi miezi ai mwaka ulikuwa hujui kuwa kuna msimu wa mvua? Acheni visingizio, fanyeni kazi kwa uaminifu," alionya.

Pia aliwataka kuacha kuchukua kazi nyingi kuzidi uwezo au kubwa kuliko uwezo wao kwa sababu ndicho kiini cha kuchelewa kukamilisha kazi.

Aliwataka kujitahidi kumaliza kazi za miradi kwa wakati au kabla ya muda wa mkataba ili kuaminiwa kupata miradi mingine.

Aliongeza kuwa wakati wa kutia saini mradi wanakuwa na ahadi nyingi za kukamilisha kwa muda husika waliokubalina lakini wakikwama, wanatoa sababu ambazo hazina msingi.

Pia alisema serikali imejipanga kuhakikisha kila mwananchi anayehamia makao makuu anapata huduma zote mhimu.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabiri Shekimweri aliwataka makandarasi waliotia saini mkataba huo wa ujezi wa miundombinu ya maji Nzuguni kuzingatia mkataba.

Shekimweri alisema atakuwa anafanya ziara za kushtukiza kila mara ili kuangalia maendeleo ya mradi huo eneo hilo na maeneo mengine.

Awali Mkurungenzi Mtendaji wa DUWASA, Aron Joseph alisema wametia saini mkataba na makandarasi wanne wenye thamani ya Sh. bilioni 4.8.

Joseph alisema kiasi hicho cha fedha kitatumika kutekeleza mradi wa visima vya maji vitano kwenye eneo la Nzuguni jijini hapa ambavyo vitatoa huduma maeneo ya Nzuguni, Ilazo na Kisasa.

Alibanisha kuwa mikataba waliyotia saini na makandarasi hao inatakiwa kutekelezwa kazi hiyo ndani ya miezi sita tangu walipotia saini rasmi hiyo jana.

Alisema huo ni sehemu ya mpango ya muda mfupi wa DUWASA kuhakikisha kila eneo la Mji wa Dodoma linapata maji safi na ya uhakika.

# Leseni za meli za uvuvi zilivyoingiza mabilioni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA kipindi cha mwezi Julai 2022 hadi Februari mwaka huu, Mamlaka ya Usimamizi Uvuvi wa Bahari Kuu imekusanya Sh. bilioni 4.1 kutokana na mapato ya utoaji leseni kwa meli za uvuvi na huduma nyingine.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Dk.Emmanuel Sweke alibainisha hayo jana jijini hapa alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa shughuli mbalimbali za mamlaka hiyo.

Dk. Sweke alisema mamlaka hiyo inalo jukumu la kutoa leseni kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu kwa meli za ndani na nje kulinda, kusimamia na kuratibu shughuli zote za uvuvi wa bahari kuu. Alisema makusanyo hayo yamevunja rekodi iliyowekwa na mamlaka hiyo kwa kipindi cha miaka saba iliyopita.

"Makusanyo makubwa ya mwisho yalikuwa ni Sh. bilioni nne katika kipindi cha mwaka 2015/16 lakini yalishuka sana baada ya kuletwa kwa kanuni ambayo ilikuwa inawataka wavuvi kutoa mrabaha wa dola 0.4 kwa kila kilo moja ya samaki.

"Hali hii ilisababisha makusanyo kushuka sana kutokana na meli nyingi za uvuvi kukimbia na kuacha kufanya uvuvi kwenye nchi yetu lakini kutokana na hali hiyo tulijifungia na kuondoa kanuni hiyo na sasa matunda yanaonekana kwa kupanda kiasi cha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na utoaji wa leseni za uvuvi na huduma nyingine zinazotolewa na mamlaka hii," alifafanua.

Dk. Sweke alisema mifumo ya kiusalama ambayo inatumiwa na mamlaka hiyo kwa sasa ina uwezo wa kuona meli zote duniani. "Mifumo hii tunayotumia sasa pamoja na kufanya doria kwa kutumia ndege, zimesaidia sana kukomesha vitendo vya uvuvi haramu bahari kuu," alisema.

Akizungumzia meli ya uvuvi iliyokamatwa na Serikali ya Tanzania mwaka 2009 ikiwa na shehena ya samaki, alisema ndiyo ilikuwa sababu kuu ya kuanzishwa kwa mamlaka hiyo mwaka 2010.

"Kabla ya kukamatwa kwa meli ile, hatukuwa na mamlaka hii lakini baada ya kukamatwa tukaona kuwa kuna haja ya kuwa na mamlaka hii ambayo ndiyo itakuwa na jukumu la kusimamia, kulinda na kuratibu uvuvi wa bahari kuu," alisema.





Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Naghenjwa Kaboyoka (wa tatu kushoto), akipokea matangazo ya Mfumo wa Kielektroniki wa Ufuatiliaji wa Hali ya Barabara kutoka kwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Barabara, Octavian Mshiu, walipotembelea ofisi za bodi hiyo, jijini Dodoma jana, kwa ajili ya kujifunza jinsi inavyotenda kazi. Wanaoshuhudia ni Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Ujenzi), Balozi Mhandisi Aisha Amour (wa pili kushoto), na Meneja wa Mfuko huo, Eliud Nyauhenga (kushoto). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TEMESA yawaita kwenye malipo wanufaika wake

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKALA wa Umeme na Ufundi Tanzania (TEMESA) umezitaka taasisi za umma zinazodaiwa baada ya kupatiwa huduma za matengenezo ya magari, mitambo, huduma za ufundi, umeme na vifaa vya kielektroniki, kulipa madeni kuwezesha wakala huo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mtendaji Mkuu wa Wakala huo, Lazaro Kilahala alitoa rai hiyo jijini hapa juzi alipozungumza katika kikao cha wadau wanaopatiwa huduma na TEMESA Mkoa wa Dodoma.

Kikao hicho kilihudhuriwa na maofisa mbalimbali wanaowakilisha taasisi za umma wakiwamo maofisa usafirishaji, maofisa kutoka serikali kuu, wizara, wawakilishi wa karakana teule zinazofanya kazi kwa pamoja na TEMESA na wazabuni wanaosambaza vipuri na vitendeakazi kwa wakala huo.

"Kulikuwa na malalamiko kwa baadhi ya wateja wanaotamani kulipa lakini changamoto ilikuwa hawaelewi wanalipaje madeni hayo na ndio sababu ya kuwaweka hawa mabalozi ili kurahisisha zoezi hili," alisema Kilahala.

Akizungumza kuhusu madeni ambayo wakala huo unadaiwa na wazabuni ambao waliikopesha vipuri miaka ya nyuma, Kilahala alisema TEMESA haipuuzii wala haijasahau kama inadaiwa na wazabuni na imeunda timu kwa ajili ya kuhakiki madeni hayo ikiwashirikisha wataalamu wake.

"TEMESA haipuuzii na wakala hauwezi kusahau kuwa unadaiwa na wazabuni, madeni yote yatalipwa, hatuwezi kufanya dhulma, kumbukeni hata Rais wetu, Dk. Samia Suluhu Hassani hapendi dhulma, anapenda haki," alisema.

Meneja wa TEMESA Mkoa wa Dodoma, Greyson Maleko, akizungumza katika kikao hicho, aliahidi wakala utaendelea kuwapatia huduma iliyo bora wakati wote na kwa ufanisi mkubwa ili watekeleze majukumu yao kwa wakati.





# Wapewa zana za kilimo kujikwamua kiuchumi

Na Nebart Msokwa, MBARALI

VIKUNDI sita vya wanawake na vijana Mbarali mkoani Mbeya, vimekabidhiwa mashamba yenye ukubwa wa zaidi ya hekta 60 kwa ajili ya kuendeleza kilimo ili wajikwamue kiuchumi.

Aidha, vikundi hivyo vimekabidhiwa zana mbalimbali za kisasa za kilimo kwa ajili ya kuendeshea shughuli hizo yakiwamo matrekta, pampu na majaketi na vifaa vingine vya kujikinga na madhara ya viuatilifu wakati wa kuhudumia mashamba hayo.

Vikundi hivyo vimepatiwa vitu hivyo na shirika lisilokuwa la kiserikali la Norges Vel ambalo linajihusisha na shughuli mbalimbali za kilimo ikiwamo usambazaji wa zana za kilimo, pembejeo na ununuzi wa mazao.

Makabidhiano ya mashamba na vifaa hivyo yalifanyiwa juzi na Mkurugenzi wa shirika hilo, Cecilia Jeremiah, aliyesema waliamua kusaidia baada ya kubaini kwamba vikundi hivyo vina uhitaji.

Alisema walibaini kwamba asilimia kubwa ya wanawake katika wilaya hiyo hawana uwezo wa kumiliki mashamba kwa kuyanunua kutokana na uhaba wa kipato.

Pia alisema kwa upande wa vijana walibaini kuwa wanapenda kilimo lakini hawana zana za kisasa za kulimia yakiwemo matrekta.

"Makundi haya ni muhimu kwenye uzalishaji lakini hayana uwezo wa kumiliki hivi vitu. Kwa hiyo sisi tumeona ni vema tuvisaidie ili viweze kushiriki vizuri kwenye kazi hii," alisema Jeremiah.

Ofisa Kilimo wa Shirika hilo, Lemana Mwampamba, alisema wamelenga kuwafikia wananchi wengi zaidi katika wilaya ya Mbarali na baadhi ya maeneo ya jirani ambayo pia makundi ya wanawake na vijana yanakabiliwa na matatizo hayo.

Alisema lengo kubwa ni kuviinua vikundi hivyo ambavyo kwa kiasi kikubwa vinazalisha mpunga wilayani hapa ili kuvisaidia kuongeza uzalishaji wa zao hilo.

Endapo vikundi hivyo vitaongeza uzalishaji, alisema vitakuwa na uwezo wa kujiongezea kipato pamoja na kuwa na uhakika wa chakula kwenye familia zao.

Baadhi ya wanachama wa vikundi vilivyonufaika na msaada huo, walilishukuru shirika hilo kwa kuvisaidia huku wakieleza kuwa vitawasaidia kujiimarisha kiuchumi.

Mmoja wa wananchi hao, Elines Mpyanga alilishukuru shirika hilo kwa kuwasaidia mashamba hayo akieleza kuwa hawajawahi kusaidiwa mashamba na taasisi yoyote hali iliyokuwa inawafanya wawe na maisha magumu.

Alisema walikuwa wanatumia fedha nyingi kwenye kukodi mashamba hali iliyokuwa inawalazimu kulima vipande vidogo vya ardhi na hivyo kutokuwa na uhakika wa kipato.

"Huu msaada utatusaidia sana, tutaongeza uzalishaji wa chakula na tunawahakikishia kwamba baada ya miaka miwili mkija hapa hamtatukuta tukiwa hivi tulivyo, mtakuta mabadiliko makubwa sana," alisema Elines.

Bahati Simon aliwaomba wakulima wengine kuwapa kazi ya kuwalimia mashamba ili vifaa walivyopewa viwasaidie kujiongezea kipato.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Ilongo, Gideoni Sichembe, aliwataka wanufaika wa msaada huo kuhakikisha wanautumia msaada huo vizuri ili kulitia moyo shirika hilo liendelee kusaidia na maeneo mengine ya wilaya hiyo.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule (katikati), akishuhudia kubadilishana nyaraka kati ya Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Dodoma (DUWASA) Mhandisi Aron Joseph (kulia) na Meneja na Ofisa miradi kampuni ya Helpdesk Engineering Tanzania, Godfrey Peter, jijini Dodoma juzi, baada ya kutiliana saini mkataba wenye thamani ya Sh bilioni 4.8 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji Nzuguni. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## RC ataka tathmini ya mifugo, malisho

Na Nebart Msokwa, MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imetoa siku 20 kwa wakuu wa wilaya zote mkoani hapa kufanya tathimini ya mifugo iliyopo katika maeneo yao na uwezo wa maeneo ya malisho yaliyotengwa ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitoa agizo hilo jana alipozungumza na wandishi wa habari na kuwataka kuwasilisha taarifa ya tathimini hiyo Februari 20, mwaka huu.

Homera alisema tathimini hiyo ni utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa hivi karibuni na Rais Samia Suluhu Hassan alipokuwa anazindua ujazaji wa maji kwenye bwawa la kuzalisha umeme la Mwalimu Nyerere la utunzaji wa mazingira.

Alisema mbali na maagizo hayo ya rais, pia yapo maagizo yaliyotolewa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kwa wakuu wa mikoa.

Alisema endapo idadi ya mifugo iliyopo kwenye wilaya itakuwa haiendani na maeneo yaliyotengwa, viongozi wa maeneo hayo watatakiwa kutafuta namna ya kukabiliana na tatizo hilo.

"Tunatakiwa kulinda mazingira yetu ikiwemo vyanzo vya maji, mkoa wetu ni muhimu sana kwenye kulinda vyanzo vya umeme ikiwemo Bwawa la Mtera, Kidatu na Bwawa la Nyerere," alisema Homera.

Alisema baada ya viongozi hao kuwasilisha taarifa ya tathimini yao, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa itaangalia namna ya kushirikiana nao kukabiliana na tatizo la mifugo.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon, wiki iliyopita alipiga marufuku wafugaji kutoka katika maeneo mbalimbali kuingiza mifugo wilayani humo kwa maelezo kuwa mifugo iliyoko ndani ya wilaya hiyo inatosheleza

# Tatizo la maji Mbega, Songwe kupatiwa suluhu

Na Nebart Msokwa, MBEYA

TATIZO la maji katika baadhi ya halmashauri za mikoa ya Mbeya na Songwe linaelekea kupata suluhu baada ya serikali kuanza mikakati ya kutekeleza mradi wa maji katika chanzo cha Mto Kiwira.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliwaambia wandishi wa habari jana kwamba mkandarasi wa kujenga mradi huo ameshapatikana na mkataba utatiwa saini kesho baina yake na Wizara ya Maji.

Alisema kampuni iliyoshinda zabuni ya kutekeleza mradi huo ni China Railway Construction Engeneering Group kwa kushirikiana na China Railway No.4 Engeneering Group ambazo ndizo zitatia saini mkataba na wizara.

Alisema awamu ya kwanza ya mradi huo itatekelezwa kwa gharama ya Sh. bilioni 99.65 bila kodi ya ongezeko la thamani na kwamba kwa kuanzia, utahudumia halmashauri mbili ambazo ni jiji la Mbeya na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Homera alisema awamu zingine za utekelezaji wa mradi huo zitakuwa za kuupanua ili uhudumie maeneo mengine yakiwamo wilaya za Chunya na Mbarali kwa mkoa wa Mbeya na baadhi ya miji ya mkoa wa Songwe ukiwamo mji wa Tunduma.

Aliishukuru serikali kwa kuamua kuanza kutekeleza mradi huu ambao ni muhimu sana kwa wananchi wa mkoa huu na utakuwa suluhisho la tatizo la maji kwetu.

"Waziri wa Maji, Juma Aweso, ndiye atakuja kutia saini mkataba huo na mkandarasi wetu na hii ni baada ya taratibu zote za ununuzi kukamilika katika wizara zote zinazohusika," alisema Homera.

Mkurugenzi wa Ufundi wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya, Mhandisi Barnabas Konga, alisema baada ya mradi huo kukamilika utaongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma hiyo kwa wananchi.

Alisema mradi huo utakuwa unazalisha lita za ujazo 117.5, hivyo kuongeza upatikanaji wa maji kutoka wastani wa lita 66.5 za sasa mpaka Lita za ujazo 184.

Konga alisema mradi huo ukikamilika utasaidia kutatua tatizo la maji kwa zaidi ya miaka 20 ijayo. Alisema kwa sasa kuna baadhi ya maeneo ambayo yalikuwa hayapati huduma kwa muda mrefu, tatizo hilo litatatuliwa.

"Mamlaka itaongeza saa za upatikanaji wa maji kutoka saa 19 za sasa mpaka saa 24 na itaongeza huduma kwa wananchi kutoka asilimia 80 za sasa mpaka asilimia 95," alisema Mhandisi Konga.

"Mradi huu ni muhimu kwa mkoa wetu kwa sababu unakuja kutatua tatizo la maji kwa muda mrefu zaidi, ikishamalizika hii awamu ya kwanza tutaanza utekelezaji wa awamu ya pili," aliongeza.

Mradi wa maji wa chanzo cha Mto Kiwira ulisanifiwa miaka kadhaa iliyopita lakini utekelezaji wake umechelewa kutokana na tatizo la upatikanaji wa fedha.





# Mwinyi afurahia ujio madaktari kutoka China

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema ujio wa timu ya madaktari bingwa kutoka China ni faraja na fursa adhimu ya kuimarisha sekta ya afya Zanzibar.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana Ikulu, Zanzibar alipozungumza na timu ya madaktari hao walioongozwa na Balozi Mdogo wa China, Ofisi ya Zanzibar, Zhang Zhisheng, chini ya kiongozi wa madaktari hao Dk. Zhao walipofika kujitambulisha.

Alisema ushirikiano uliopo baina ya China na Zanzibar ni wa kihistoria na wa muda mrefu na aliishukuru serikali ya China kwa kuendelea kuiunga mkono Zanzibar hususan kwenye sekta ya afya, kwa msaada wa vifaa vya kisasa na teknolojia mpya ya kufanya operesheni bila upasuaji na huduma zingine za uchunguzi na kitabibu.

Rais Mwinyi aliwapongeza madaktari hao kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuwahudumia wananchi kwa kuwatibu kwa kutumia utaalamu wa kisasa.

Alisema madaktari hao mbali ya kutoa mbinu za kibingwa pia wanasaidia maeneo mbalimbali ya afya ikiwamo kutoa vifaa vya kisasa kwenye hospitali hizo, utaalamu kwa madaktari wazawa na kuweka miundombinu sawa ya hospitali. Dk. Mwinyi aliiomba serikali ya China kuisaidia Zanzibar madaktari bingwa na serikali imejiimarisha zaidi kwenye sekta ya afya kwa kuongeza hospitali za wilaya Unguja na Pemba, hivyo akawaomba madaktari hao kuongeza nguvu na utaalamu kwenye hospitali hizo.

Balozi Zhang alimpongeza Rais Mwinyi kwa kuiongoza Zanzibar kuwaletea maendeleo wananchi wake na kueleza wanashuhudia mafanikio makubwa yaliyofikiwa na serikali.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, aliishukuru timu ya madaktari hao kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali na kukubali kujitoa kuongeza nguvu kuimarisha sekta ya afya nchini.

Mkurugenzi wa Tiba katika Wizara ya Afya, Dk. Msafiri Marijani, alisema madaktari hao ni wataalamu wa masuala ya masikio, pua na koo (ENT), upasuaji kwa kinamama bila kupasua, macho, meno, uzazi na magonjwa mengine ya kinamama. Pia wamo wataalamu wa mionzi na wa uchunguzi wa magonjwa ya kansa pamoja na wakalimani. Watakuwapo Zanzibar kwa mwaka mmoja wakishirikiana nao kwenye Hospitali za Mnazi Mmoja na Abdalla Mzee, Pemba pamoja na kuongeza nguvu na utaalamu kwa hospitali za Kivunge na Chake Chake kisiwani Pemba.

Dk. Marijani alieleza mafanikio makubwa yamepatikana kutokana na ujio wa madaktari wao mbali na matibabu kwa wananchi lakini kuanzishwa kitengo cha madaktari bingwa watakaofanya oparesheni bila ya kumpasua mgonjwa katika hospitali za Mnazi Mmoja na Abdalla Mzee.

Alisema kwa mara ya kwanza Mnazi Mmoja wametumia upasuaji bila kupasua ambao ulifanikiwa kwa kiasi kikubwa, na kusifu vifaa vipya vya kitaalamu kutoka kwa timu hiyo aliyoieleza kwamba imeongeza uweledi na ufanisi wa hali ya juu.

Kiongozi wa timu ya madaktari hao, Dk. Zhao aliishukuru serikali ya Zanzibar na uongozi wa Wizara ya Afya kwa ushirikiano waliowaonesha tokea wamefika Zanzibar mwezi Septemba mwaka jana pamoja na kusifia ukarimu wa watu wa Zanzibar.

Dk. Zhao ambae pia ni mtaalamu wa upasuaji wa magonjwa yote, alisema kipindi kifupi walichofika Zanzibar kwa ushirikiano wa madaktari wenyeji wa Mnazi Mmoja na Abdalla Mzee wametibu wagonjwa wengi wa maradhi mbalimbali na kutibu kesi nyingi zilizokuwa zikiwasumbua wananchi wa Zanzibar waliofika vituo humo kwa ajili ya matibabu.

Alisema uwapo wao utapunguza kesi nyingi zinazowasumbua wananchi na kuwataka kuitumia fursa ya uwepo kwa kufika kwa wingi kwenye hospitali za umma ili wapate matibabu na ushauri wa kitaalam.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza na madaktari wa Kichina waliofika Ikulu jijini Zanzibar juzi, kwa ajili ya kujitambulisha wakifuatana na Balozi Mdogo wa China anayefanyia kazi kisiwani humo, Zhang Zhisheng (wa pili kulia). **PICHA: IKULU**

## SMZ yaweka vipaumbele kuendeleza uchumi wa bluu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mgeni Hassan Juma, amesema serikali imeweka vipaumbele vya kuendeleza miundombinu inayowezesha matumizi endelevu ya bahari kwa lengo la kuweka mazingira bora ya uwekezaji kwa maslahi ya Watanzania.

Mgeni alisema hayo jana wakati akifungua mkutano wa mapitio ya maandalizi ya program mpya ya Uchumi wa Buluu Tanzania uliofanyika Hoteli ya Golden Tulip, Mjini Magharibi.

Alisema mpango huo wa maendeleo wa mwaka 2050 utapunguza umaskini na kukuza uchumi kwa manufaa ya wananchi.

Serikali kupitia Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi, alisema imewashirikisha wanawake katika uchumi huo na wanaitumia bahari katika kilimo cha mwani, ufugaji wa majongoo bahari na ufugaji wa kaa.

Alisama program ya uchumi wa bluu ni jumuishi inayohusisha maendeleo na ushiriki wa sekta binafsi na wanawake katika usimamizi wa bahari.

"Jambo hili linakwenda sambamba na malengo ya serikali katika utekelezaji wa majukumu ya kuthamini mchango na ushirikishwaji wa sekta binafasi katika kuleta maendeleo", alisema.

Aidha, alisema sekta binafsi ni moyo katika ukuaji wa uchumi Tanzania hivyo kuna kila sababu ya kuwasilisha wadau mbalimbali katika kutekeleza mpango huo.

Katibu Mkuu Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi, Aboud Suleiman Jumbe, alisema mchakato wa mradi huo utasaidia katika kuwanyanyua wananchi wa Zanzibar katika kuwapatia elimu, ubunifu, nyenzo, miundombinu, fursa za mahitaji ya masoko katika uwekezaji wa sekta binafsi na kuimarisha usawa wa kijinsia na jamii.

Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) Christine Musisi, alisema Zanzibar kupitia Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi ina mwamko wa kuwasikia wadau katika kuimarisha uchumi wa bluu ili uwe endelevu na kuleta tija kwa wananchi.

# Mkakati upatikanaji maji kukamilika karibuni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Maji, Nishati na Madini, Hassan Kaduara, katika kutatua tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama, serikali imeanzisha miradi mbalimbali na baadhi inatarajiwa kukamilika mwaka huu. Kaduara aliyasema hayo jana katika mkutano wa majadiliano juu ya kuangalia tatizo la maji uliowashirikisha watendaji wa wizara na washirika wa maendeleo, uliofanyika Maisara.

Alisema tatizo la maji linatokana na mambo mbalimbali ikiwamo uchakavu wa miundombinu kutokana na kuwa ya zamani ambayo ni kabla ya mwaka 1964.

"Miundombinu ya maji ni chakavu licha ya kuwa na uhaba wa maji lakini pia uchakavu huo unaweza kusababisha athari za kiafya, hivyo tunabadilisha miundombinu hiyo," alisema.

Pia aliwataka wananchi kuendelea kuwa wavumilivu lakini kwa wale wanaopata huduma hiyo, kulipa bili ili kuiwezesha serikali kusambaza maji maeneo mingine. Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Joseph Kilangi, alisema serikali inatarajia kuifanyia marekebisho Sera ya Maji Zanzibar ya mwaka 2004, ili kuwa na sera rafiki itakayoisaidia Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ambayo imebeba majukumu makubwa na kusambaza maji kwa jamii mijini na vijijini.

Alisema tayari wameshapatiwa fedha na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) ambazo zinatumika kuifanyia marekebisho sera hiyo ambayo inatarajiwa kukamilika ndani ya miezi sita ijayo.

Kwa mujibu wa Kilangi, hatua hiyo inafanyika baada ya kuona kuna changamoto kubwa ya maji kila mahali ikiwamo upotevu wa maji na kusababisha maji mengi yanayozalishwa kupotea katika maeneo ambayo si rafiki.

Pia alisema uharibifu wa mazingira unatokana na mabadiliko ya tabianchi na Serikali itatafuta wafadhili watakaosaidia kuhifadhi vyanzo vya maji.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**VICTOR SAULI OLOTU** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye usajili namba: **MC167 BVX**, CHASSIS NAMBA: **LTBPK8BG88H2K05709** na ENGINE NAMBA: **KL162FMJ7J05709.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/55468/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DAUDI A. KAJIGILI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina **ya TOYOTA COROLLA** yenye usajili namba : **T 851 AAM,** CHASSIS NAMBA: **AE1000279231** na ENGINE NAMBA: **5AH148434.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **WMB/RB/MBWENI**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**RAMADHAN ATHUMAN MKANDWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 297 BAV** aina ya **BOXER,** Chassis No. **md2a21bz1dwk49937.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/53440/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SILASVAN ISAWEN KWEKA** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T711AHN** aina ya Toyota Corolla ,Chassis No. **EE 980058331,** Engine No. **3E0725093** Atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi **ARU/ARU/RB 56272/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TANGA**

**Kituo cha MJINI TANGA Mkoa TANGA**

**Usimamizi wa mirathi na 24|2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MARIAM AMOUR AWADHI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**

**YALIOLETWA NA GHANIA MABROUK RASHID NA SARA FRANCIS VESSO**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama zamwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa Hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 13 Mwezi 02 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehem anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

Imetotewa leo tarehe 08 Mwezi 02 mwaka 2023

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
TANGA MJINI

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**Probate and Administration Cause No.11 of 2023**

**In the matter of the Estate of the late ALOYCE SIMON MWOGOFI**
**Of Nzuguni within Dodoma City**

**And**

**In the matter of an application for letters of administration by AGNETH CHALES NG'ANDE and TRIFONIA ALOYCE MWOGOFI.**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before the 16 Day of 02, 2023
Dated at Dodoma this 06 day of 02, 2023

RESIDENT MAGISTRATE


**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042,**

**DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Rwanda yaishutumu DRC kuwa kigeugeu

**KIGALI,** Rwanda

RAIS wa Rwanda Paul Kagame (pichani), amemshutumu kiongozi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) Felix Tshisekedi, kwa kutoheshimu makubaliano kadhaa ya kushughulikia mzozo unaosababisha mapigano mashariki mwa nchi hiyo.

Mvutano kati ya majirani wa eneo la Maziwa Makuu, unaendelea kuongezeka huku DRC ikiishutumu Rwanda kwa kuvamia eneo lake kwa kutumia waasi wa M23.

Katika hotuba yake kwa mashirika ya kidiplomasia nchini Rwanda, Kagame alimkosoa Tshisekedi kwa kushindwa kushughulikia suala la ndani la nchi yake na kisha kuilaumu Rwanda.

Hata hivyo, serikali ya DRC haijajibu matamshi hayo ya Rais Kagame.



"Mtu huyu amevunjia heshima mikataba mingi aliyofanya na watu ikiwa ni pamoja na hata mara ya mwisho mjini Bujumbura", alisema Kagame.

"Tunajadili mambo hadharani, alishiriki, tuliandika taarifa, kuwapa watu yale tuliyojadili na njia ya kusonga mbele. Taarifa hiyo inasomwa, lakini siku inayofuata taarifa iliyo kinyume inasomwa Kinshasa." Aliongeza.

Mkutano wa wakuu wa nchi za Afrika mashariki mwishoni mwa juma lililopita mjini Bujumbura, Burundi, ulielekeza kusitishwa mara moja na kujiondoa kwa makundi yote ya kigeni na kuwepo mazungumzo kati ya pande zote.

Siku moja baadaye, msemaji wa serikali ya Congo alisema wanatii makubaliano ya Novemba huko Luanda kumaliza mzozo huu.

Rais Kagame alisikitishwa na kwamba suala la waasi linaendelea kurudi nyuma kwa takriban miongo mitatu sasa licha ya Umoja wa Mataifa kuwa na zaidi ya walinda amani 10,000 waliotumwa kushughulikia hilo. **BBC**

# Waliofariki kwa tetemeko la ardhi Uturuki wafikia 12,000

**ANKARA,** Uturuki

IDADI ya vifo kutoka nchi za Uturuki na Syria, vilivyotokana na tetemeko la ardhi, inatarajiwa kuongezeka na kufikia zaidi ya 12,000 wakati zoezi la uokoaji likiendelea.

Mpaka sasa mamia ya majengo yaliyoporomoka katika miji mingi hayajafikiwa na kuwa makaburi ya watu waliokuwa wamelala wakati tetemeko hilo lilipotokea.

Katika mji wa Uturuki wa Antakya, imeshuhudiwa maiti zikiwa zimefunikwa kwa blanketi na shuka na nyingine zikiwa kwenye mifuko ya miili, zilipangwa chini nje ya hospitali.

Hata hivyo, mkazi mmoja aliyejulikana kwa jina la Melek (64), alilalamikia ukosefu wa timu za uokoaji. "Tulinusurika na tetemeko la ardhi, lakini tutakufa hapa kutokana na njaa au baridi."

Wengi katika eneo la maafa walikuwa wamelala ndani ya magari yao au mitaani chini ya blanketi kwenye baridi kali, wakihofia kurejea kwenye majengo yaliyotikiswa na tetemeko hilo la kipimo cha 7.8, ambalo lilikuwa baya zaidi nchini Uturuki tangu 1999. Na kufuatia tetemeko kubwa la pili saa chache baadaye.

**Zaidi ya watu 298,000 wamekosa makazi na makazi 180 ya muda kwa watu waliokimbia makazi yao yamefunguliwa.**

Nchini Uturuki, idadi ya vifo vilivyothibitishwa viliongezeka hadi 9,057 mpaka jana, Syria ilipanda hadi kufikia 2,950, kulingana na maelezo ya serikali na vitengo vya huduma ya uokoaji.

Maofisa wa Uturuki walisema kuwa watu milioni 13.5 waliathirika katika eneo hilo linalochukua kilomita 450 kutoka Adana magharibi hadi Diyarbakir mashariki.

Nchini Syria, watu waliofariki wanatoka kusini mwa Hama, kilomita 250 kutoka kitovu cha tetemeko.

Baadhi ya waliofariki Uturuki walikuwa wakimbizi kutoka vita vya Syria. Mifuko ya miili yao ilifika mpakani kwa kutumia teksi, magari ya kubebea mizigo na malori ya gorofa ili kupelekwa maeneo yao ya asili kwa ajili ya kuzikwa.

Zaidi ya watu 298,000 wamekosa makazi na makazi 180 ya muda kwa watu waliokimbia makazi yao yamefunguliwa.

Aidha, nchini Syria, juhudi za kutoa misaada zinatatizwa na mzozo ambao umegawanya taifa hilo na kuharibu miundombinu yake.

Usambazaji wa msaada wa kibinadamu wa Umoja wa Mataifa kupitia Uturuki kwa mamilioni ya watu wa kaskazini-magharibi mwa Syria unaweza kuanza tena baada ya operesheni ya muda mrefu kusitishwa.

Katika mji wa Aleppo nchini Syria, wafanyakazi katika hospitali ya Al-Razi walimhudumia mtu aliyejeruhiwa ambaye alisema ndugu zake 12 akiwemo mama yake na babaake walikufa wakati jengo walilokuwa wakiishi lilipoporomoka. **BBC**



Wakaazi wakimwokoa msichana aliyejeruhiwa kutoka kwenye vifusi vya jengo lililoporomoka nchini Syria. **PICHA: AFP**

# Kamatakamata viongozi wa zamani Kenya yaleta hofu

**NAIROBI,** Kenya

WAZIRI wa Mambo ya Ndani wa Kenya, Kithure Kindiki, amekanusha madai kwamba maofisa wa polisi walitumwa kumkamata waziri wa zamani wa mambo ya ndani Fred Matiang'i nyumbani kwake usiku wa juzi.

Katika taarifa kwa vyombo vya habari, Kindiki alisema madai hayo ni ya uwongo.

"Tumepokea ripoti za vyombo vya habari kuhusu madai ya uvamizi wa makazi ya waziri wa zamani wa mambo ya ndani Dk. Fred Matiang'i' na watu wasiyojulikana jana usiku, ni uongo," alisema waziri huyo.

Mawakili wa Dk. Matiang'i na baadhi ya wanasiasa waliozungumza kutoka eneo la tukio walidai kuwa watu hao walikuwa maofisa wa polisi waliotumwa kumkamata aliyekuwa Katibu wa Baraza la Mawaziri.

"Madai haya ni ya uongo mtupu. Hakuna ofisa wa polisi au ajenti yeyote wa usalama kutoka taasisi au idara yoyote ya Serikali aliyetumwa nyumbani kwa Dk. Matiang'i kumkamata, kumnyanyasa au kuingilia haki zake za Kikatiba kwa namna yoyote ile," alisema Kindiki.

Katika hatua nyingine, Matiang'i, amekimbilia mahakamani akidai kuvamiwa na polisi usiku wa manane nyumbani kwake eneo la Karen.

Mawakili wa Matiang'i waliripoti mahakamani jana kwamba polisi walijaribu kumkamata mteja wao kinyume cha sheria.

Mawakili hao walidai kuwa baadhi ya maofisa wa polisi watiifu kwa Waziri huyo wa zamani walimdokezea kuhusu kukamatwa kwake na hivyo kusababisha atoe tahadhari.

Matiang'i aliiomba mahakama kutoa maagizo ya kuwazuia polisi kumkamata au kumfungulia mashtaka. **BBC**

# KAGERA SUGAR MECHI SABA BILA USHINDI

**Na Adam Fungamwango**

SULUHU iliyoipata Kagera Sugar Jumatatu iliyopita dhidi ya wenyeji wao Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Ushirika, Moshi, Kilimanjaro imeifanya kutimiza mechi saba bila kupata ushindi wowote kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mara ya mwisho kwa timu hiyo inayofundishwa na Mecky Mexime kushinda ilikuwa ni Desemba 2 mwaka jana ilipoifunga Ihefu mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera.

**Kwenye mechi hizo saba, imetoa sare tano na kupoteza mbili.**

Baada ya ushindi wake dhidi ya Ihefu ilichapwa mabao 2-0 dhidi ya Dodoma Jiji na bao 1-0 dhidi ya Singida Big Stars, suluhu dhidi ya Polisi na Coastal Union, sare ya mabao 2-2 dhidi ya Geita Gold na Azam FC, sare ya bao 1-1 dhidi ya Simba.

"Mechi ile ilikuwa tushinde kabisa, lakini kuna mambo madogo madogo tu, utulivu tu umekosekana na hili ndilo linalotusumbua sana," alisema Mexime.

"Tulijua Polisi watacheza hivi, watakuja kupiga mipira mirefu kutushinikiza, kwa hiyo tuliingia na mfumo ambao uliwadhibiti, niliwaambia wachezaji wangu tukipata mpira tucheze tu kwenye nafasi na kweli tukafanikiwa.

"Lakini tatizo kubwa umakini na utulivu tu sehemu ya kumalizia," aliongeza Mexime ambaye alirejeshwa katikati ya Oktoba kuchukua nafasi ya kocha Francis Baraza ambaye alitimuliwa baada ya matokeo mabaya ya timu hiyo.

Kagera Sugar inakamata nafasi ya nane kwa pointi zake 26 ikicheza mechi 22 mpaka sasa.




Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi wa Benki ya CRDB, Stephen Adili (kulia) akikabidhi jezi kwa Mwakilishi wa Kurugenzi ya Michezo ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Kanali John Thomas Nyanchoha, jijini Dar es Salaam ikiwa ni sehemu ya udhamini wa vifaa vya michezo katika mashindano ya Baraza la Majeshi (BAMATA 2023) yanayotarajiwa iliyoanza mkoani Mtwara jana. Benki hiyo, imekabidhi vifaa mbalimbali vya michezo vyenye thamani ya Sh milioni 11. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Bares ataka pointi sita Februari hii*

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Tanzania Prisons, Mohammed Abdallah 'Bares' (pichani), amewekwa wazi kuwa anataka pointi sita katika michezo miwili ya Ligi Kuu Tanzania Bara kwa Febuari hii ili kujiondoa kwenye hatari kwenye msimamo.

Bares amesema anahitaji kushinda mechi hizo mbili za ugenini dhidi ya Polisi Tanzania na Coastal Union ili kujiweka katika nafasi nzuri na kujiondoa katika Play Off.

Prisons inashika nafasi ya 13 ikiwa tayari imecheza michezo 22, kushinda tano na wamepoteza mechi 10 wakikusanya pointi 22 katika msimu huu ambao wako katika hali mbaya.

Akizungumza na gazeti hili jana, Bares alisema anaendelea kukinoa kikosi cha timu yake kufikia malengo yao ya kutafuta pointi tatu muhimu katika mechi hizo mbili za ugenini ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kuendelea kubaki kwenye ligi.

Alisema nafasi waliyopo sasa sio salama kwa sababu wasipokuwa makini kutafuta pointi katika michezo hiyo ya ugenini watakuwa katika mazingira magumu ya kujinasua kutoka chini ya msimamo.

"Sio mgeni kwenye ligi ya Tanzania, tuko katika nafasi ya Play Off, tunatakiwa kutoka hapo na lazima tushinde mechi zilizopo mbele yetu, mipango iliyopo sasa ni kushinda michezo yetu hii miwili ya mwezi huu ambayo tutakuwa ugenini," alisema Bares.



Alisema ligi imekuwa na ushindani, kila mechi kwao ni muhimu na wachezaji wanatambua wanahitaji kufanya kazi kubwa ya kutafuta alama katika kila mchezo ili kufikia malengo hasa katika michezo hiyo miwili ya mwezi huu.

Bares alisema ana imani na wachezaji wake kupambania timu katika michezo iliyopo mbele yao na kupata matokeo mazuri katika kila mechi iliyopo mbele yao kabla ya Machi ambapo wanakibarua kingine ugenini dhidi ya Namungo FC.

## Kundemba kufa au kupona kwa Polisi leo

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Kundemba FC leo inahitaji kushinda mchezo wake dhidi ya Maafande wa Polisi SC ili kujiondoa katika hatari ya kushuka daraja kwenye Ligi Kuu ya Zanzibar ukiwa ni mzunguko wa 20.

Kundemba ipo nafasi ya 11 ikiwa na alama 20 wakati Polisi ipo nafasi ya 13 ikiwa na alama 16 huku wakiwa tayari katika mstari wa hatari wa kushuka daraja.

Katika mchezo huo ambao unatazamwa kuwa mchezo mgumu kwa kuwa timu zote zinahitaji alama tatu ili kujiondoa nafasi za chini katika msimamo wa Ligi hiyo yenye timu 16 huku timu nne zitashuka daraja mwisho wa msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili Kocha Mkuu wa Kundemba, Ali Vuai Shein alisema amekiandaa kikosi chake kucheza kwa kujituma ili kuhakikisha wanashinda mchezo huo.

Alisema nafasi waliyopo ya 11 sio nzuri kwao kwa sababu timu nne kutoka chini zinautofauti wa alama ndogo, hivyo lazima washinde mchezo huo ili wazidi kujiondoa katika hatari.

Alisema anajua mchezo huo utakuwa mgumu kwa kuwa wapinzani wao nao wanahitaji alama tatu ili kuhakikisha wanajitoa katika mstari mwekundu wa kushuka daraja.

## Minziro aipigia hesabu Ruvu Shooting

**Na Hadija Mngwai**

KOCHA Mkuu wa Geita Gold, Fred Ferix Miziro anaipigia hesabu kali mechi yake dhidi ya Ruvu Shooting ya Februari 17 kuhakikisha anaibuka na pointi tatu.

Geita Gold ambayo ipo nafasi ya 5 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa imecheza michezo 22 ilijikusanyia pointi 31, na imejipanga kumaliza Ligi katika nafasi nne za juu kama ilivyokuwa msimu uliopita wa 2021/22 ilipopata nafasi kucheza michuano ya kimataifa.

Akizungumza na Nipashe, Minziro amesema kuwa, amejipanga kuhakikisha anapata matokeo mazuri katika mechi nane zilizobakia ikiwemo dhidi ya Ruvu Shooting ili kumaliza katika nafasi nne za juu katika msimamo wa Ligi Kuu Bara.

"Mzunguko wa pili wa Ligi Kuu ni mgumu kuna ushindani mkubwa nahitaji kufanya vizuri katika mechi nane zilizobakia ili kuweza kupata pointi katika kila mchezo na niweze kumaliza katika nafasi nzuri mwisho wa Ligi," alisema Minziro.

"Natarajia kucheza na Ruvu Shooting katika mchezo wangu unaofuata Februari 17 na tunaendelea na maandalizi kuelekea mchezo huo kuhakikisha tunapata matokeo mazuri.

## ZISIKUPITE

### BRANTHWAITE AVUTIA

LIVERPOOL ni miongoni mwa Klabu zinazovutiwa na mlinzi wa Everton, Jarrad Branthwaite mwenye umri wa miaka 20, ambaye yuko kwa mkopo PSV Eindhoven.

### SILVA MKATABA MPYA

CHELSEA ipo kwenye mazungumzo ya mwisho mwisho na Thiago Silva kuhusu mkataba mpya wa mlinzi huyo wa Brazil ambaye Septemba atatimiza umri wa miaka 39. ***(London Evening Standard)***

### ALVAREZ AWINDWA

ARSENAL, Liverpool na Newcastle United zote zinavutiwa na kiungo wa kati wa Ajax na Mexico, Edson Alvarez mwenye umri wa miaka 25. ***(Caught Offside)***

### ZUBIMENDI ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL pia inaweza kuingia katika mbio za kutaka kumnunua kiungo wa kati wa Real Sociedad, Martin Zubimendi mwenye umri wa miaka 24 msimu huu kutokana na Barcelona kuelekeza nguvu zao za uhamisho kwingine. ***(Mirror)***

### JUDE AZIDI KUGOMBEWA

KIUNGO wa kati wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19, ameripotiwa kukataa kuhamia Chelsea na Paris St-Germain msimu wa joto. Liverpool, Barcelona, Real Madrid, Manchester City na Manchester United nazo zinamtaka mchezaji huyo. ***(Express)***

### BETO AWANIWA EVERTON

KLABU ya Everton itafanya jaribio lingine la kumnunua mshambuliaji wa Ureno, Beto, 25, kutoka Udinese ya Italia msimu wa joto baada ya kushindwa kufikia makubaliano Januari. ***(Mondo Udinese)***

### IRAOLA AIKATAA LEEDS

LEEDS United imekataliwa na kocha wa Rayo Vallecano, Andoni Iraola, 40, kuchukua nafasi ya Jesse Marsch aliyetimuliwa huku timu hiyo ya Ligi kuu England ikikabiliwa na hali ngumu zaidi katika kujaribu kumteua kocha mpya. ***(Onda Cero, via Express)***

### FOSTER KUTUA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inaweza kumsajili mlinda mlango wa zamani wa Manchester United na England, Ben Foster, 39, kama mbadala wa Hugo Lloris ambaye atakuwa nje kwa angalau wiki sita kutokana na jeraha la goti. Foster alitangaza kustaafu Septemba mwaka jana lakini anaweza kujiunga kwa mkopo wa muda mfupi. ***(Mirror)***

### JONG, FATI WATAKIWA MAN

KLABU ya Manchester United ipo katika harakati za kumnunua kiungo wa kati wa Barcelona na Uholanzi, Frenkie de Jong, 25, na mshambuliaji wa Hispania, Ansu Fati mwenye miaka 20. ***(Mundo Deportivo, via Mail)***

### GIROUD MKATABA MPYA

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Arsenal, Olivier Giroud, 36, anatarajiwa kujadili mkataba mpya na AC Milan. Mchezaji huyo alikuwa akisakwa na Everton Januari. ***(Fabrizio Romano)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# AUBAMEYANG SASA KUTIMKIA MAREKANI

**LONDON,** England

Ni baada ya kutoswa na Chelsea katika kikosi cha Ligi ya mabingwa Ulaya na kocha...

KURUDI kwa Pierre-Emerick Aubameyang kwenye Ligi Kuu ya England hakukwenda kama alivyotarajia na sasa mambo yanaonekana kumuendea kombo.

**Mshambuliaji huyo raia wa Gabon alirejea England baada ya kuondoka kule kule Barcelona, akisisitiza kwamba alikuwa na uhakika wa kuthibitisha ubora wake baada ya kuondolewa kikatili pale Arsenal.**

Lakini mtu aliyefanikisha kuwasili kwake, kocha Thomas Tuchel alifukuzwa na Chelsea na nafasi yake ikachukuliwa na Graham Potter ambaye ameonesha wazi kutomhitaji Aubameyang.

Alimwondoa kwenye kikosi chao cha Chelsea cha Ligi ya Mabingwa Ulaya ili kutoa nafasi kwa wachezaji wapya waliotua kikosini hapo.

Na sasa kwa mujibu wa Le10 Sport la Ufaransa, Aubameyang yuko "karibu sana" kuondoka pale Stamford Bridge na muelekeo wake ni katika Klabu ya Los Angeles FC ya nchini Marekani.

Ripoti hiyo imesema kwamba, Los Angeles na Chelsea tayari zimefikia makubaliano, na Aubameyang anaweza kuondoka haraka kwenye Ligi Kuu ya England.

Aubameyang atahamia katika Klabu ya Los Angeles inayoshiriki Ligi Kuu ya Marekani, MLS, kwa mkopo, na hivyo kuruhusu The Blues hao kuokoa kiasi kikubwa cha mshahara wake.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,074,7

MECHI KALI
AC MILAN
VERSUS
TORINO
1 | 1.77
X | 3.46
2 | 4.44

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# BENZEMA FITI FAINALI KLABU BINGWA YA DUNIA

**RABAT,** Morocco

CARLO Ancelotti anatumaini Karim Benzema atakuwa fiti kuichezea Real Madrid katika fainali ya Kombe la Klabu bingwa ya Dunia.

Benzema ambaye ni mshindi wa tuzo ya Ballon d'Or mwaka jana hakwenda Morocco mapema wiki hii kwa ajili ya michuano hiyo, baada ya kupata jeraha la misuli ya paja.


Hata hivyo, kocha Ancelotti baada ya Madrid kuishinda Al Ahly 4-1 katika nusu fainali ya michuano hiyo Jumatano, alithibitisha kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35 atasafiri kwenda kufanya mazoezi na wachezaji wenzake Ijumaa.

Benzema ataungana na Eder Militao, ingawa Ancelotti ambaye alithibitisha Marco Asensio na Dani Carvajal waliwekwa benchi dhidi ya Al Ahly kutokana na matatizo ya utimamu wao - ametia shaka zaidi uwezekano wa beki huyo kuwepo kwenye mchezo wa fainali wa Jumamosi dhidi ya Al-Hilal.

"Hawajapona kabisa," alisema Ancelotti akiwaambia waandishi wa habari kuhusu Benzema na Militao.

"Karim anaendelea vizuri na kuna mashaka zaidi kuhusu Militao. Watafanya mazoezi Ijumaa halafu tutaona.

"Carvajal alikuwa na homa na Asensio alizidiwa kidogo. Nadhani atakuwa tayari kwa mchezo wa Jumamosi."



# Martinez, Courtois na Bounou wawania golikipa bora wa Fifa

**PARIS,** Ufaransa

MSHINDI wa Kombe la Dunia 2022, Emiliano Martinez anakabiliwa na ushindani kutoka kwa Thibaut Courtois na Yassine Bounou katika kuwania tuzo ya golikipa bora wa mwaka wa Fifa wa Wanaume.

Awali makipa watano waliteuliwa kuwania tuzo hiyo, ambayo inatambua uchezaji bora zaidi wa makipa katika soka ya wanaume katika kipindi cha kati ya Agosti 8, 2021 na Desemba 18, 2022, wakati Martinez alipoisaidia Argentina kushinda Kombe la Dunia kwa mara ya tatu kwenye historia ya nchi hiyo.

Wachezaji wawili wa Ligi Kuu ya Brazil, Alisson na Ederson walikosa orodha ya mwisho kufuatia kura iliyopigwa kati ya makocha na manahodha wa timu za kimataifa, waandishi wa habari na mashabiki.

Mchango mkubwa wa Martinez katika ushindi wa fainali ya Kombe la Du-
nia wa Argentina dhidi
Ufaransa ulimweka mi
goni mwa walio mstari
mbele kuwania tuzo hi
ambayo itatolewa kat
hafla ya utoaji wa tuzo
Fifa mjini Paris baada
mwezi huu.

Mchezaji huyo mwen
umri wa miaka 30 aliok
mkwaju muhimu na ku
nyima Randal Kolo Mua
bao la ushindi katika mu
wa ziada katika sare ya 3
kabla ya kuokoa mkwa
wa Kingsley Coman wal
ti Argentina ikishinda k
mikwaju ya penalti.

741,067/-

# BURUDANI ZAFANIKISHA KAMPENI ZA WAJIKI

**Na Sabato Kasika**

NGOMA za asili, maigizo, ngonjera na mashairi, ni miongoni mwa burudani zilizosaidia katika kampeni ya kuhamasisha vita dhidi ya rushwa ya ngono kwa wanafunzi na wasichana.

Kampeni hiyo ilizinduliwa rasmi jijini Dar es Salaam mwaka jana na zilihitimishwa hivi karibuni, ambapo ziliendeshwa katika Wilaya za Kinondoni, Ilala na Temeke zikiratibiwa na Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI).

Mkurugenzi Mtendaji wa WAJIKI, Janeth Mawinza alisema walitumia vikundi mbalimbali vya burudani ambavyo vilisaidia kukusanya watu kupata elimu ya kupambana na rushwa hiyo.

**"Miongoni mwa vikundi hivyo, kilikuwa ni cha ngoma za asili cha Mnaa Theatre na vingine, tulivyoshirikiana navyo kwenye kampeni hii, kwa ajili ya kuepusha wanafunzi na rushwa hiyo inayowanyemelea," alisema Mawinza.**

Alifafanua kuwa kampeni hiyo ilifanyika shuleni, mitaani na kwenye vijiwe vya madereva wa bodaboda, daladala na bajaj, kwa madai kwamba hao ndio wamekuwa wakituhumiwa kuwarubuni wanafunzi kwa lifti.

"Women Fund Tanzania (WFT), walitufadhili katika kampeni hii ambayo lengo lake lilikuwa ni kunusuru wanafunzi na mabinti kwa ujumla ili watambue mbinu zinazotumiwa na madereva hao na kuzikwepa," alisema.

Aliongeza kuwa mbali na njia hiyo, nyingine walizoitumia ni mikutano na mijadala, mabango, stika zenye ujumbe wa kukemea rushwa hiyo, mitandao ya kijamii kama Facebook, Instagram, tovuti na vyombo vya habari zikiwamo redio, magazeti, TV, Online TV.



Janeth Mawinza alipokuwa katika moja ya kampeni hizo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## *Nabi apata mbinu kuiua*

INATOKA UKURASA 24

sia.

Alisema baada ya mechi yao na Namungo FC waliangalia wapi panapohitajika kuimarishwa na kufanyia kazi mapungufu yao ikiwemo sehemu ya kiungo.

"Tumefanya maandalizi mazuri tunatambua mchezo utakuwa wa ushindani mkubwa kwa sababu tuko ugenini na tunahitaji kupata alama katika mchezo wetu huo wa kwanza katika hatua ya makundi," aliongeza.

Kikosi cha Yanga kipo jijini Tunis kikiwa kimefikia kwenye Hotel ya nyota tano ya Golden Tulip tayari kwa ajili ya mchezo wao huo wa Jumapili.

## Simba SC yaahidi ushindi Guinea bila Ntibazonkiza

INATOKA UKURASA 24

aliongeza kocha huyo.

Mosses Phiri ambaye kwa muda mrefu alikuwa majeruhi, amesafiri na kikosi hicho akiweka wazi kama atapata nafasi ya kucheza ana hamu ya kuwafurahisha wanachama na mashabiki wa Simba.

"Niko fiti na ndiyo maana unaniona nakwenda na kikosi. Wachezaji ambao majeruhi kama Saido, Augustine Okrah na Peter Banda wameachwa, nina furaha nimerudi kikosini na kama nitapata nafasi ya kucheza basi nataka kuwafurahisha wanachama na mashabiki wa Simba kwa sababu mshambuliaji kazi yake ni kufunga na kwenye mechi hii lengo letu ni kupata ushindi kwa sababu ukiupata kwenye mechi ya kwanza unajiweka vema kwenye kundi na mnatengeneza ari na kujiamini zaidi," alisema straika huyo raia wa Zambia.

Kwa upande wake Sakho alisema kama mambo yatakwenda kama yalivyopangwa basi wanatarajia ushindi kwa sababu lengo si kushinda bali ni kufuzu na kusonga mbele kwenye kundi hilo.

Awali wanachama na mashabiki wa Simba walikuwa na wasiwasi labda Saido ameachwa kutokana na kuwepo jina lake kwenye kikosi cha Geita Gold kilichoshiriki michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika msimu huu, lakini Ofisa Habari wa klabu hiyo Hemed Kivuyo alisema hawakufanikiwa kuliingiza jina la Saido kwa sababu walichelewa.

"Jina la Saido halipo kwenye orodha ya wachezaji wa Geita Gold walioshiriki Kombe la Shirikisho kwa sababu ni kweli nia ilikuwepo, lakini tulichelewa, hatukufanikiwa kuliingiza," alisema Kivuyo.

Kocha msaidizi wa Simba, Juma Mgunda amesema kuwa, nyota wa timu hiyo wapo na molari ya hali ya juu kuelekea mchezo wao dhidi ya Horoya na kuhakikisha wanapata ushindi.



# SUPA JACKPOT
# MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 11/02/23 | 18:00 | Southampton FC vs Wolverhampton Wanderers | 2.75 | 3.10 | 2.60 |
| 02. 11/02/23 | 18:00 | KVC Westerlo vs KAA Gent | 2.80 | 3.30 | 2.42 |
| 03. 11/02/23 | 18:15 | UD Almeria vs Real Betis Seville | 2.80 | 3.30 | 2.44 |
| 04. 11/02/23 | 22:45 | Lazio Rome vs Atalanta BC | 2.27 | 3.35 | 3.00 |
| 05. 11/02/23 | 23:00 | Valencia CF vs Athletic Bilbao | 2.95 | 3.15 | 2.41 |
| 06. 12/02/23 | 09:00 | Macarthur FC vs Wellington Phoenix FC | 2.55 | 3.15 | 2.29 |
| 07. 12/02/23 | 15:00 | Toulouse FC vs Stade Rennes | 3.05 | 3.35 | 2.25 |
| 08. 12/02/23 | 16:00 | Getafe CF vs Rayo Vallecano | 2.75 | 2.85 | 2.80 |
| 09. 12/02/23 | 16:30 | Vitesse Arnhem vs FC Utrecht | 2.39 | 3.45 | 2.75 |
| 10. 12/02/23 | 17:00 | Angers SCO vs AJ Auxerre | 2.25 | 3.30 | 3.10 |
| 11. 12/02/23 | 17:00 | Montpellier HSC vs Stade Brest 29 | 2.35 | 3.25 | 2.95 |
| 12. 12/02/23 | 17:30 | Hertha BSC vs Borussia Monchengladbach | 2.75 | 3.50 | 2.37 |
| 13. 12/02/23 | 18:15 | RC Celta de Vigo vs Atletico Madrid | 3.40 | 3.05 | 2.24 |
| 14. 12/02/23 | 19:30 | 1. FC Cologne vs Eintracht Frankfurt | 2.65 | 3.45 | 2.47 |
| 15. 12/02/23 | 20:30 | Real Valladolid vs CA Osasuna | 2.60 | 3.05 | 2.80 |
| 16. 12/02/23 | 21:00 | Sporting Lisbon vs FC Porto | 2.75 | 3.20 | 2.55 |
| 17. 12/02/23 | 22:45 | Olympique Lyon vs RC Lens | 2.39 | 3.40 | 2.80 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## IJUMAA - 10/02/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 1958 | Gasogi United vs Rutsiro FC | 1.88 | 2.95 | 4.35 |
| 16:00 | 2700 | Lillestrom vs Ham-Kam | 1.55 | 4.36 | 4.46 |
| 16:00 | 4544 | Magara Young Boys vs Olympic Star | 1.94 | 3.22 | 3.64 |
| 16:00 | 4990 | Ajax Cape Town vs Baroka FC | 1.97 | 3.16 | 3.63 |
| 17:00 | 2839 | JSM Skikda vs MO Constantine | 3.06 | 2.85 | 2.37 |
| 17:00 | 3105 | US Chaouia vs Ain M'lila | 1.50 | 3.15 | 6.40 |
| 17:00 | 3526 | Delhi Dynamos FC vs Hyderabad FC | 3.16 | 3.32 | 2.07 |
| 17:00 | 4137 | Ib Khemis El Khechna vs USM Annaba | 1.97 | 2.80 | 4.25 |
| 17:00 | 4408 | ES EL Ghozlane vs CA Batna | 1.60 | 3.32 | 5.81 |
| 18:00 | 1996 | Universitatea Cluj vs CS Mioveni | 1.93 | 3.16 | 4.10 |
| 18:00 | 3188 | Radnik Surduluca vs Mladost Lucani | 2.36 | 3.15 | 2.79 |
| 18:00 | 4526 | MC Alger vs JS Saoura | 2.01 | 2.65 | 3.85 |
| 19:00 | 2970 | Ranheim vs Stjordals-Blink | 1.49 | 4.47 | 4.89 |
| 19:00 | 3338 | Dinamo Zagreb vs Istra | 1.29 | 4.88 | 8.51 |
| 19:00 | 3480 | Spartak Moscow vs Sochi | 1.83 | 3.54 | 3.69 |
| 19:00 | 3762 | Ghazl EL Mahallah vs Arab Contractors | 3.44 | 2.79 | 2.34 |
| 19:15 | 4691 | Al Nasr Dubai vs AL Khaleej Khor Fakkan | 1.64 | 3.83 | 4.34 |
| 20:30 | 2312 | Maritzburg Utd vs Kaizer Chiefs | 4.55 | 3.31 | 1.73 |
| 20:30 | 2537 | Arminia Bielefeld vs Hansa | 2.22 | 3.28 | 3.08 |
| 20:30 | 5844 | Karlsruher SC vs Greuther Furth | 2.45 | 3.37 | 2.67 |
| 21:00 | 5062 | SCU Torreense vs Moreirense | 3.15 | 3.20 | 2.20 |
| 21:00 | 5642 | Omonia Nicosia vs Aris Limassol | 2.35 | 3.31 | 2.93 |
| 21:00 | 5930 | Rapid Bucuresti vs U Craiova SA | 1.94 | 3.17 | 4.01 |
| 21:30 | 5285 | Neuchatel Xamax vs Lausanne-Sport | 3.00 | 3.47 | 2.09 |
| 22:00 | 1657 | Always Ready vs Libertad Gran Mamore | 1.08 | 8.29 | 19.68 |
| 22:00 | 1788 | FC Eindhoven vs Almere City | 2.38 | 3.26 | 2.79 |
| 22:00 | 2001 | OH Leuven vs Cercle Brugge | 2.40 | 3.34 | 2.79 |
| 22:00 | 3078 | NAC Breda vs De Graafschap | 2.74 | 3.32 | 2.39 |
| 22:00 | 3790 | Maastricht vs FC Oss | 1.93 | 3.47 | 3.57 |
| 22:00 | 3803 | AZ Alkmaar vs SBV Excelsior | 1.21 | 6.32 | 10.87 |
| 22:00 | 4536 | VVV Venlo vs Heracles Almelo | 3.47 | 3.63 | 1.92 |
| 22:00 | 5605 | PEC Zwolle vs Jong AZ Alkmaar | 1.26 | 5.66 | 8.81 |
| 22:00 | 5644 | Den Bosch vs Jong Ajax | 2.78 | 3.51 | 2.27 |
| 22:15 | 4079 | FC Aarau vs Yverdon-Sport FC | 2.01 | 3.64 | 3.06 |
| 22:30 | 1543 | Wisla Krakow vs Resovia Rzeszow | 1.70 | 3.61 | 4.23 |
| 22:30 | 2722 | Genoa vs Palermo | 1.70 | 3.44 | 4.97 |
| 22:30 | 4120 | Sturm Graz vs Rapid Vienna | 1.84 | 3.42 | 3.78 |
| 22:30 | 4919 | Schalke 04 vs VfL Wolfsburg | 3.51 | 3.61 | 1.93 |
| 22:45 | 1171 | AC Milan vs Torino | 1.77 | 3.46 | 4.44 |
| 22:45 | 1496 | Eupen vs Mechelen | 2.63 | 3.42 | 2.48 |
| 22:45 | 2489 | Hamilton vs Hearts | 6.01 | 4.09 | 1.45 |
| 22:45 | 2545 | Brugge vs Union Saint Gilloise | 2.30 | 3.39 | 2.89 |
| 22:45 | 3393 | Derry City vs Shamrock Rovers | 2.32 | 3.21 | 2.80 |
| 22:45 | 5536 | Larne vs Glenavon | 1.27 | 5.07 | 8.49 |
| 23:00 | 3131 | Cadiz CF vs Girona | 2.86 | 3.16 | 2.47 |
| 23:00 | 3201 | Nice vs AC Ajaccio | 1.55 | 3.80 | 6.00 |
| 23:00 | 3596 | Granada vs Tenerife | 2.06 | 3.07 | 3.72 |
| 23:00 | 3852 | Birmingham vs West Bromwich | 3.42 | 3.32 | 2.06 |
| 23:00 | 5168 | Newry City AFC vs Carrick Rangers | 2.46 | 3.41 | 2.49 |
| 23:15 | 1160 | FC Vizela vs GD Chaves | 1.81 | 3.53 | 4.18 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Ijumaa Februari 10, 2023
Nipashe



Aubameyang kutimkia Marekani UKURASA 21

# Nabi apata mbinu kuiua US Monastir

●●● Kikosi kimeondoka nchini leo na matumaini huku jezi mpya...

Na Saada Akida

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi juzi alikuwepo uwanjani kushuhudia mchezo wa Ligi Kuu ya Tunisia ili kuwasoma wapinzani wao, US Monastir ambao watacheza nao kwenye mechi ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika, Jumapili.

**Nabi alikuwepo kwenye dimba la Stade Ahmed Khouaja, mjini Tunis akishuhudia mchezo wa Ligi Kuu kati ya wapinzani wao US Monastir wakiwa ugenini dhidi ya Rejiche, ambapo walishinda 2-0, mabao yake yakifungwa na Idrissa Mhirsi dakika 10 na Bassam Deli dakika ya 30.**

Nabi pia alifanikiwa kushuhudia mchezo mwingine kabla ya huo kwenye Ligi wakati Monastir walipofungwa bao 1-0 na Ben Guerdan kwenye uwanja wa Mustapha Ben Jannet.

Yanga watakuwa ugenini kusaka pointi tatu muhimu katika mchezo wao huo utakaopigwa, Uwanja wa Olympique Hammadi Agrebi, katika mji huo mkuu wa Tunisia.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema amepata muda mzuri wa kuwatazama wapinzani wao Monastir katika michezo miwili waliyocheza kwenye ligi hiyo na kuona ubora na madhaifu yao.

Alisema amewaona wachezaji hatari ambao wanatakiwa kuwachunga na sehemu gani wako bora na wataingia katika mchezo wao wa kwanza wa hatua ya makundi kwa tahadhari kubwa.

"Tumeona ubora wa kikosi cha wapinzani wetu kwa kushuhudia michezo yote miwili ya ligi kuu nchini humu, wachezaji gani ni hatari na wanaotakiwa kuchungwa tunapokutana nao," alisema Nabi wakati akizungumza na gazeti hili kutoka nchini Tuni-

INAENDELEA UKURASA 23



Kocha wa Yanga, Nasreddine Nabi. **PICHA: MAKTABA**

## Simba SC yaahidi ushindi Guinea bila Ntibazonkiza

**Adam Fungamwango na Hadija Mngwai**

KIKOSI cha wachezaji 24 wa Simba kilichoondoka nchini alfajiri ya jana kwenda nchini Guinea kwa ajili ya mechi ya kwanza ya Kundi B hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa barani Afrika dhidi ya Horoya Jumamosi ijayo, huku ikimuacha kiungo mshambuliaji wao tegemeo kwa sasa, Saido Ntibazonkiza, lakini ikiahidi ushindi.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Roberto Aliveira amesema kuwa wanakwenda kucheza mechi muhimu kwa klabu, wanachama na mashabiki wa Simba kwenye michuamo hiyo ya kimataifa, lakini akiahidi kufanya vema, huku winga Pape Sakho akisema wanachoangalia si mechi hiyo tu, bali ni kuvuka kwenye hatua hiyo ya makundi.

"Tunakwenda kucheza mechi ya mashindano ya kimataifa, ni muhimu kwa klabu na sote pia, nadhani kuna muda mrefu kabla ya mechi kuamua nani atacheza na nani hatocheza kwenye kile kikosi cha wachezaji 11," alisema Roberto.

"Kuna wengine tumewaacha, kwenye mpira huwezi kutumia wachezaji wote kwenye mchezo mmoja, mfano tumemuacha Saido Ntibazonkiza ni mchezaji muhimu sana kwenye kikosi changu, lakini ni majeruhi nitawatumia wachezaji wengine waliokuwepo, ni mchezaji mzuri, lakini wengine watanipa kile ninachokitaka.

Simba ni timu kubwa na ina wachezaji wengi wazuri ambao wanaweza kucheza na kuipa matokeo mazuri,"

INAENDELEA UKURASA 23

## Benzema fiti fainali Klabu Bingwa ya Dunia

**RABAT,** Morocco

CARLO Ancelotti anatumaini Karim Benzema atakuwa fiti kuichezea...

HABARI UK. 22




## Martinez, Courtois wawania golikipa bora wa Fifa

**PARIS,** Ufaransa

MSHINDI wa Kombe la Dunia 2022, Emiliano Martinez anakabiliwa na...

HABARI UK. 22



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >